

ENENDENI, MKAWAAMBIE



...kushuhudia, na maskini dada huko nyuma, nafikiri inaelezea wimbo huo:

Loo, upendo wa Mungu, ni tajiri na safi jinsi gani!

Jinsi usivyoweza kupimika na una nguvu!

Ni siku ya jinsi gani kwetu! Hebu kwa utulivu tu, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, tumwimbie Bwana huo kabla tu ya maombi. Hebu, Teddy, tafadhali, tupe sauti kidogo. Na hebu tuuimbe tu kwa... huku vichwa vyetu vimeinamishwa, macho yetu yamefungwa, kabla tu ya maombi.

Loo, upendo wa Mungu, jinsi ulivyo tajiri na safi!

Jinsi usivyoweza kupimika na una nguvu!

Milele... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

² Kama wino, maji yote yangaligeuka kuwa wino, na mbingu zote zifanywe ngozi ya kuandikia, na kila shina duniani liwe unyoya wa kuandikia, na kila mwanadamu kazi yake iwe ni uandishi, hata hivyo isingeweza kuelezea upendo wa Mungu kwa jamii ya Adamu iliyoanguka. Tunakushukuru Wewe, Baba, kwa ajili ya Damu hiyo ya thamani ya Bwana Yesu, na kwa ajili ya asubuhi hiyo ya kumbukumbu ya ule ufufuo, na kwa ajili ya pendo Lako la ukombozi lililokwisha kumiminwa katika mioyo yetu leo hii, na Roho Mtakatifu. Likituleta katika ushirika pamoja na Yeye, Yule wa Kiungu, Muumba. Akituleta katika udugu, duniani, ambao haujawahi kushindwa. Hakuna chama, hakuna nadhiri, ingaliweza kamwe, kamwe kulinganishwa na udugu wa wanaume na wanawake waliozaliwa mara ya pili. Na utakuwa milele ni wimbo wa watakatifu na malaika!

³ Tunaomba leo hii ya kwamba utabariki yote tufanyayo katika kujaribu kuelezea, shu—shukrani zetu mioyoni mwetu Kwako, kwa ajili ya yale uliyotufanyia. Na kujua ya kwamba si kwamba tu mioyo ya wanafunzi ilifurahishwa asubuhi hiyo, Mariamu na Mariamu Magdalene, lakini sisi pia, wanafunzi Wako leo hii, mioyo yetu inafurahishwa ile saa tunapoona kwamba Yeye hajafa, bali yu hai. Jalia daima abaki hai mioyoni mwetu, miongoni mwetu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Kamwe kusingeweza kuwa na mtu yeyote angaliweza kuuelezea huo ufufuo!

⁴ Sasa, kwenye asubuhi hii ya ufufuo, ni wakati wa ajabu sana kwa matukio madogo kutukia kanisani sasa, hiyo ni, akina mama wakiwaweka wakfu watoto wao wachanga. Ni jambo

jipya, kitu fulani kimeongezewa nyumbani mwao. Baraka mpya zimewajia. Nao wanataka, kama malipo, kumkabidhi Mungu.

⁵ Halafu baada ya u—ujumbe wa asubuhi, tutakuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa, mpate kufufuliwa kutoka kwa magonjwa yenu, mpate afya mpya. Ndipo mara baada ya hayo, kwa wale ambao hawajabatizwa, tutakuwa na ufufuo wa huo; tuzikwe majini, kufufuka kwenye upya wa maisha. Kwa jumla ni ufufuo asubuhi ya leo, ufufuo! Mioyo yetu imefanywa kufurahi na ni myepesi, tunapoziimba hizi nyimbo na kusikiliza shuhuda za wengine, juu ya asubuhi hii ya ajabu sana ya ufufuo. Ndipo tunaangalia nje na kuona Mungu ameifurahia, miti inafufuka.

⁶ Siku moja, huko chini Kentucky, mimi na Bw. Wood tulikuwa tukiwinda kuchakulo, nasi tukaenda kwenye eneo la mtu fulani. Mtu huyo huenda ameketi hapa sasa hivi, nijuavyo mimi. Naye alidhaniwa kuwa ni kafiri. Basi Ndugu Wood akamwuliza, kasema, “Naweza kuwinda kuchakulo kwenye eneo lako?”

Akasema, “Naam, Wood, unaweza kuwinda kuchakulo. Rudi nyuma tu.”

Akasema, “Vema, nilikuja na mchungaji wangu.”

⁷ Ndipo akasema, “Wood, usiniambie kwamba umekuwa duni sana hata inakubidi kubebana na mhubiri wakati wote!”

⁸ Na kwa hiyo akaniita huko apate ku—kunitambulisha. Naye huyo jamaa alikuwa amesema yeye kidogo alikuwa ni jamaa mgumu. Aliambiwa na wengine, hivyo, lakini asingeweza kuona kitu chochote cha kumfanya aamini.

⁹ Basi kulikuwako na mtofaa uliosimama pale ambao nilikuwa nimeokota tofaa kutoka kwake. Ilikuwa ni Agosti. Ndipo nikamwambia huyo muungwana, nikasema, “Huo mti una umri gani?”

¹⁰ Naye akasema, “Kama miaka thelathini,” kitu kama hicho. Alikuwa ameupanda.

¹¹ Nami nikasema, “Umekula matofaa tangu umekuwa ukizaa?”

“Naam, bwana.”

¹² Nikasema, “Ni kitu gani kinachoupata mti huo? Ikiwa utauangalia, sasa ni Agosti, hali ya hewa imekuwa joto kote; lakini sasa majani yanapukutika kutoka kwenye mti huo, nao utomvu unaondoka kwenye matawi, ukiingia chini kwenye mizizi. Kama ungekaa huku juu kwenye kipindi chote cha baridi kali, huu mti usingekuwako tena; bali unaingia chini katika udongo, ukajifiche na upepo mwanana baridi. Kama ungalikaa huku juu, ungekufa, usingezea matofaa tena. Lakini unashuka chini ukajifiche mizizini, upate kurudi mwaka ujao, kukuletea matofaa kadhaa kutoka mahali fulani, na majani kadhaa.”

¹³ Kisha nikasema, “Sasa, bwana, na—naomba uniambie ni Akili gani inayoufanya utomvu huo kuondoka mtini kabla ya hali yoyote ya hewa baridi, na kushuka chini mizizini ukajifiche? Kama unaweza kuniambia ni kitu gani kinachosababisha hayo, na unielezee, kinachofanya hivyo, basi nitakuacha uweke mkono wako juu ya Mungu.” Nikasema, “Hebu weka maji kwenye nguzo uone kama yatafanya hivyo, uone kama mabadiliko ya misimu yatafanya hivyo. Kuna Akili fulani kuu inayoushusha utomvu huo chini kwenye mzizi wa mti, kisha inaupandisha tena ukiwa na uhai mpya. Huyu ni Mungu.”

¹⁴ Naye akasema, “Kamwe sijahudhuria kanisa sana.” Akasema, “Lakini kulikuwa na mhubiri aliyekuwa huku Acton, wakati mmoja, na kumwambia mwanamke fulani, aliyeshi kilimani, ambaye dada yake alikuwa mkutanoni usiku huo, naye akamwambia alikuwa akimwomba dada aliyekuwa na kansa.” Naye akasema, “Mimi na mke wangu tulikuwa tumeenda kule kumsaidia.” Kisha kasema, “Alikuwa mahututi sana, kwa kansa ya tumboni, hata iliwabidi kumgeuza kitandani kwa shuka, na kadhalika. Dada yake akairudisha hiyo lesa,” kasema, “baada ya huyo mtu kumwambia kuhusu hali yake na kila kitu, kasema ‘iweke hiyo lesa juu yake.’” Kisha kasema, “Yeye ni mzima leo hii.”

¹⁵ “Basi inaonyesha tu,” nikasema, “Akili ile ile iliyouambia utomvu huo mtini, mwaka baada ya mwaka, moja kwa moja machoni penu, kushuka kuingia kwenye mizizi na kujificha, ilikuwa ndiyo Akili ile ile iliyoniambia kwamba huyo mwanamke angeponywa wakati alipoweka ile. . .” Nikasema, “Hilo si—si la kisiri sana. Una mhubiri bora zaidi aliyesimama kwenye kitalu chako cha mbele, huo mti, anayekwambia mwaka baada ya mwaka.”

¹⁶ Kama tukiangalia tu pande zote, tunamwona Mungu kila mahali. Yuko kwenye kila mti, kila jani la unyasi. Hakuna kitu kinachoweza kusababisha hilo ila Mungu. Tunaweza kufanya kitu kinachofanana nalo; bali si uhai huo, ni Mungu.

¹⁷ Sasa, jani dogo la nyasi limeongezwa kwenye makazi kadhaa hapa, nasi tunataka kuwaweka wakfu maskini watoto hao wachanga kwa Bwana. Teddy, tunao wimbo mdogo hapa tunaoimba, *Waleteni*, tafadhali ucheze tu huo wakati akina mama wanaotaka watoto wao wachanga wawekwe wakfu, na akina baba, watawaleta watoto wao hapa juu madhabahuni.

¹⁸ Basi tuna maua mengi madogo ya Pasaka hapa madhabahuni asubuhi ya leo, sivyo? Jamani, jamani! Nawazia kunao watoto akina Mariamu, akina Ruthu, akina Rebeka, maskini Yakobo, Paulo na Yohana, wote hapa pote, maskini maua madogo ya Pasaka kwa ajili ya kizazi kingine.

¹⁹ Ni sawa, papo hapo. Ninaamini Ndugu Beeler anataka kupiga picha hii ya jamaa hu—huyu mdogo aliyesimama hapa,

ni—ni mjukuu wa Ndugu Wood, Dada Wood hapa. Na wengine wanakuja sasa pamoja na watoto wao. Njoni moja kwa moja, jamani. Hiyo ni sawa. Ndugu Neville.

²⁰ Umoja wa ndoa takatifu ni mkuu, umeamriwa na Mungu. Na kupitia ndoa takatifu watoto hawa wachanga vipenzi wanazaliwa.

²¹ Itakubidi kuniambia jina lake hapa sasa. Brenda Sue. Unaonekana tofauti kabisa, mtoto mchanga, kuliko nilipokuona kwanza. Vema, huyu hapa mtoto Brenda Sue Wood, kweli ni hazina ndogo ya thamani kwa mioyo yetu sote, na hasa sana kwa mama huyu mchanga na baba.

²² Na katika nyakati za Biblia, watu wengi huwanyunyizia watoto hawa wachanga, ila sisi tunajaribu kufuatilia mwelekeo wa Biblia kwa karibu sana tuwezavyo, kamwe hatukuona ambapo walipata kunyunyiziwa, katika Biblia, ila waliletwa kwa Bwana Yesu Naye akawabariki. Nasi tunawachukua, kama watumishi Wake, na kuwainua Kwake.

²³ Ninaamini ya kwamba mnajua jinsi babu yake anavyomjivunia, mwajua. Kwa hiyo na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu.

²⁴ Bwana Yesu, Mtoto wa Mungu, Yule aliyetolewa kwa ajili ya dhambi zetu. Na ni jambo la thamani sana kuwaona watoto wadogo wakiletwa Kwako, katika kumbukumbu ya yale yaliyotukia miaka mingi iliyopita, wakati akina mama na baba walipowaleta watoto wao Kwako. Tumeshika mbele Zako, leo hii, katika mikono ya imani, mtoto Brenda Sue Wood, ambaye ametumwa katika familia ya Ndugu yetu David na mke wake wa thamani. Baba Mungu, mbariki mtoto huyu.

²⁵ Wanakiri imani yao Kwako, wakati wakimwasilisha mtoto wao wa ndoa yao. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utawabariki. Basi jalia mioyo yao ipashwe moto na Roho Mtakatifu, kuishi maisha ya kitauwa sana, yaliyowekwa wakfu, hata mtoto huyu mchanga atalelewa katika makazi ya Kikristo, alelewe katika maonyo ya Mungu, na kuishi maisha marefu, yenye furaha hapa duniani, na kukutumikia Wewe siku zote za maisha yake. Na Utukufuni, ambako familia zinakusanyika humo, jalia mtoto Brenda Sue na baba yake na mama, na watu wao wote, wakusanyike kukizunguka kiti cha enzi cha Mungu, wamekombolewa kwa neema ya Kristo, ambaye tunamwinua Kwake sasa.

²⁶ Dada yangu mdogo, sasa nakukabidhi kwa Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya maisha ya utumishi Kwake, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina.

²⁷ Mungu akubariki, Marilyn, David, furaha tele na ufanisi. Mjalie huyu mtoto mdogo auishie Ufalme wa Mungu.

²⁸ Sasa, huyu hapa mvulana mzuri, tabasamu kubwa mno usoni mwake. Jina lake? [Mama anajibu. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Sharon Rose. . . [Mama yake anasema, “Sharon Daulton.”—Mh.] Daulton. Daulton. Je, huyu ni mtoto wa Ndugu Ed? Vema, kwa namna fulani, yapata miaka ishirini na miwili iliyopita, Mungu alichukua kutoka mikononi mwangu mtoto Sharon Rose, ambaye yuko Mbinguni, leo hii. Na sasa, kumkabidhi Yeye, huyu hapa Sharon Rose Daulton. Tunamjua Ndugu Ed na Dada Daulton, hapa, kama rafiki zetu wapendwa. Mtoto wa kupendeza jinsi gani!

Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe huyu mtoto Sharon Rose. Katika kumbukumbu ya Bwana Yesu mkuu, Yule aliyesimama duniani, nao wakamletea wasichana wadogo kama huyu, Ninamwombea mtoto huyu mchanga, Bwana. Jalia aishi na awe na nguvu na afya. Jalia aishi kwa utukufu wa Mungu. Wabariki baba na mama yake. Jalia alelewe katika maonyo ya Mungu. Wanakiri imani yao Kwako wakati wakimkabidhi mtoto wao mchanga Kwako. Sasa tunakupa Wewe, mtoto Sharon Rose Daulton, kwamba utayabariki maisha yake, Bwana. Ninamkabidhi kutoka mikononi mwa mama na baba yake, Kwako, Bwana na Mwokozi Wangu, Yesu Kristo, kwa ajili ya Utukufu Wake. Amina.

Mungu akubariki, dada, na wewe, ndugu.

Loo, jamani! Maskini mvulana mdogo, mgonjwa. Shida yake ni ipi? [Mama yake anasema, “Kichwa chake kinakuwa kikubwa kupita kiasi.” Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kitu tofauti. Ninamwamini.

Bwana, Mungu, ninamshikilia Kwako mtoto Mason. Ninaomba, Bwana Yesu, ya kwamba utamchukua mtoto huyu mchanga ninayemshika humu ndani mikononi mwangu, kumweka wakfu Kwako. Ninalaani mateso haya juu yake. Katika Jina la Yesu Kristo, mtoto Mason na awekwe mikononi Mwako, Bwana, na jalia haya mateso yamwache. Huyu mtoto na aishi kwa heshima na utukufu wa Mungu. Hawa wazazi wanaonyesha imani yao wakati wakimleta. Naomba umponye huyu mtoto na kumpa afya. Na aishi kwa utukufu wa Mungu, kukutumikia Wewe. Bwana Mungu, nakupa mtoto Mason, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya maisha yake na kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Amini tu kwa moyo wako wote.

Loo, msichana mdogo, pia? Vema, hilo ni sawa. Njoo huku, jamaa mdogo. Simama papa hapa. Jina lako ni. . . ? [Baba anasema, “Sumner.”—Mh.] Sumner. Ndugu na Dada Sumner. Ninaamini unatoka Georgia, sivyo? Nilidhani nilikumbuka maombi. Kuna watu wengi huko chini. Huyu ni. . . [“Latrell.”]

Latrelle. ["Dwight."] Dwight. ["David."] Na David. Umesikia jina lao. Mungu na ayaandike majina yao kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.

Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea maskini vipenzi hivi asubuhi ya leo, wakati nikiweka mkono wangu juu ya misokoto midogo kichwani mwao, nywele ndogo nyororo za wavulana hawa. Ee Bwana, wabariki. Wazazi wao wameonyesha upendo na imani yao Kwako kwa kuwakabidhi watoto wao. Nasi tunawaweka wakfu Kwako, Bwana, wakati tumewatoa mikononi mwa wazazi wao, wapate kusimamishwa hapa kwenye madhabahu hii asubuhi ya leo, kuyaweka maisha wakfu kwa Mungu. Wabariki, Baba. Tunaomba ya kwamba utawajalia kuishi wawe na furaha, siku zote za maisha yao, Uzima wa Milele katika ulimwengu ujao. Jalia walelewe katika maonyo ya Mungu, katika makazi ya Kikristo.

Sasa, kwa agizo la Yesu Kristo, alivyotoa mfano kwa wahudumu Wake, kwamba wanapaswa kufuata kama vile Yeye amefanya, ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Huko chini kabisa katika mkoa wa mwangaza wa jua wa Georgia, mtoto huyu mchanga aliletwa hapa na baba na mama yake wapendwa, apate kuwekwa wakfu Kwako kwenye asubuhi hii ya kumbukumbu. Ni kumbukumbu ya neema Yako katika familia yao. Ninaomba ya kwamba utambariki mtoto Renee, mama na baba yake. Nao wanaonyesha imani yao Kwako, kwa kumleta huyu mtoto, wakitaka baraka Zako juu yake. Basi jalia aishi na awe Mkristo hodari, mwenye furaha, siku zote za maisha yake; na awe na Uzima wa Milele katika siku zijazo, katika ulimwengu ujao. Lijalie, Baba. Kama vile ulivyovichukua vitu vitamu kama hivi, kama watoto hawa asubuhi ya leo, mikononi Mwako mwenyewe, hizi familia zimeonyesha imani yao Kwako, kwa kuwaleta kwa watumishi Wako. Nasi tunambariki mtoto Renee na kumkabidhi Kwako; kutoka mikononi mwa wazazi wake, Kwako. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba umbariki. Amina.

Ubarikiwe, ndugu. Mungu akubariki, Renee.

Hebu tuimbe tu kifungu kimoja cha huo.

Waleteni, waleteni,

Waleteni kutoka maeneo ya dhambi;

Waleteni, waleteni,

Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.

²⁹ Loo, jinsi ningalipenda kusimama mstarini na kuzungumza kuhusu kila mmoja wa hao jamaa wadogo, lakini mimi ni mwenda pole sana, kwa vyovyote vile, nao watu wamesimama. Ndugu Wood aliniambia asubuhi ya leo, akasema mgongo wake ulikuwa ukiuma, kutokana na kusimama. Hamjui

jinsi ninavyowathamini ninyi kusimama na kungojea! Nami nitauharakisha tu huu ujumbe, jinsi iwezekanavyo. Nanyi sikilizeni kwa makini sana.

³⁰ Sikuwa na wakati wa kutayarisha ibada ya asubuhi ya leo, ama ujumbe huu asubuhi ya leo, dakika moja tu. Nilichagua fungu la maneno na kitu fulani kilichokuwa tofauti.

³¹ Basi katika Pasaka iliyopita nilihubiri juu ya somo: “*Alipoishi*, Yeye alinipenda. *Alipokufa*, akaniokoa. *Alipozikwa*, aliziondolea dhambi zangu mbali sana. *Alipofufuka*, akanihesabia haki bure milele. Siku moja Yeye *Yuaa*, loo, siku yenye utukufu!”

Halafu asubuhi ya leo tulihubiri juu ya somo: *Najua*.

³² Na sasa, Bwana akipenda, ninataka kusoma kutoka mlango wa Marko Mtakatifu. Nanyi muombe pamoja nami sasa.

³³ Na mara baada ya hili itakuwa ni ibada ya uponyaji. Halafu baada ya ibada ya uponyaji itakuwa ni ibada ya ubatizo. Na halafu ibada zitakuwa usiku wa leo saa moja na nusu.

³⁴ Sasa Marko 16.

Hata sabato ilipokwisha kupita, Mariamu Magdalene, . . . Mariamu mama ya Yesu, na Salome, walikuwa wameleta manukato, wapate kwenda kumpaka.

. . . alfajiri mapema, siku ya kwanza ya juma, wakaenda kaburini, jua lilipoanza kuchomoza.

Wakasemezana wao kwa wao, Ni nani atakayetwingirishia lile jiwe mlangoni pa kaburi?

Hata walipotazama, waliona ya kuwa lile jiwe limekwisha kuingirishwa: nalo lilikuwa kubwa mno.

Wakaingia kaburini wakaona kijana ameketi upande wa kuume, amevaa vazi refu jeupe; wakastaajabu.

Na wakawaambia . . . Naye akawaambia, Msiogope: Mnamtafuta Yesu Mnazareti, aliyesulibishwa: amefufuka; hayupo hapa: patazameni mahali walipomweka.

Lakini enendeni zenu, mkawaambie wanafunzi wake na Petro kwamba awatangulia kwenda Galilaya: huko ninyi mtamwona, kama alivyowaambia.

Wakatoka nje upesi, wakakimbia kutoka kaburini; maana walitetemeka na kushangaa: wala hawakumwambia mtu neno; maana waliogopa.

Naye Yesu alipofufuka alfajiri siku ya kwanza ya juma, alimtokea kwanza Mariamu Magdalene, ambaye kwamba alimtoa pepo saba.

Huyo akashika njia akawapasha habari wale waliokuwa naye, naye...nao wakali wanaomboleza na kulia.

- 35 Mnaona, walikuwa kwenye lundo la majivu, pia.

Walakini hao, waliposikia kama yu hai, naye amemwona, hawakusadiki.

- 36 Jinsi Maneno ya Mungu yalivyo ya kisiri!

Baada ya hayo akawatokea wengine...watu wawili miongoni mwao, ana sura nyingine, nao walikuwa wakishika njia kwenda shamba.

Na wakati...na hao wakaenda zao wakawapa habari wale wengine: wala hao hawakuwasadiki.

Baadaye akaonekana na wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa ugu...kwa—kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu.

Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote,...hubiri Injili kwa kila kiumbe.

Aaminiye na kubatizwa ataokoka;...asiyeamini, atahukumiwa.

Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; Katika jina langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya;

Watashika nyoka;...wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa,...watapata afya.

Basi Bwana alipokwisha kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.

Nao wale wakatoka, wakihubiri kote kote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kuthibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nao. Amina.

- 37 Ningetaka kuchukua somo kutoka kwa maneno mawili: *Enendeni, Mkawaambia.*

- 38 Mnajua, haifai kitu sana kwenda endapo huna kitu cha kuwaambia. Nafikiri hiyo imekuwa ndiyo shida kubwa sana siku hizi. Tunaenda kuwaambia, tunaenda bali hatuna kitu cha kuwaambia, hakuna kitu cha kuwafaidi, hakuna kitu kingaliweza kuwasaidia watu.

- 39 Lakini kama tutafuata maagizo kama wanafunzi hawa waliopata lile agizo, sisi tunalo agizo lile lile, “Enendeni, mkawaambie wanafunzi Wangu ya kwamba nimefufuka katika wafu.” Enendeni, mkawaambie hilo!

- 40 Kisha anasema, “Enendeni, mkalihubiri, na kuonyesha ishara hizi kwamba Mimi ni hai kutoka kwa wafu.” Ni

ujumbe wa jinsi gani! “Enendeni, mkawaambie, na mwende, mkawaonyeshe wanafunzi Wangu mambo haya mliyoona, kwamba sijafa, bali nimefufuka kutoka kwa wafu.”

⁴¹ Katika Ujumbe wa asubuhi asubuhi ya leo, tuliona kwamba kila mmoja wetu ana lundo dogo la majivu ya matatizo na majaribu ambapo tunaketi tumetulia juu yake, wakati mwingine, tukiingojea faraja. Tuliona ya kwamba yule mzee wetu mkuu Ayubu aliona ono, kwa sababu hawakuwa wamepata Pasaka bado, bali aliona miaka elfu nne mbele asubuhi ya leo. Aliona miaka elfu nne mbele, Pasaka, na kupaza sauti, katika dhiki yake, “Najua Mkombozi wangu yu hai! Siku za mwisho, Yeye atasimama juu ya nchi. Ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuangamiza mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu.”

⁴² Sasa, baada ya Pasaka, tunaona ya kwamba Mungu alimpa mwanadamu agizo, “Enendeni, mkawaambie! Na kama mkiwaambia, *hizi* zitafuatana nanyi. Nendeni na kuwaambia!”

⁴³ Sasa, haifai kitu, kama nilivyosema, kwenda, kwenda, isipokuwa uwe na kitu cha kuwaambia. Na iwapo una ujumbe mbaya wa kuwaambia, basi hautafaa kitu. Inakupasa kuwaambia siri ni nini.

⁴⁴ Wakati fulani uliopita nilikuwa nikisoma kitabu, juu ya mvulana mdogo aliyekuwa... aliyeingia katika mashindano. Na katika shindano hili yeye alikuwa ajipatie jina maarufu. Mvulana yeyote mdogo angeweza kuweka hilo neno la siri akilini mwake mpaka atakapofika mahali fulani, naye angelitamka hili neno la siri, ndipo mlinda lango angemruhusu apite. Hiyo ilikuwa ni kupima akili asilia ya huyo mtoto. Naye alipofika mahali hapo, akinena hayo maneno ya siri aliyopewa, lango lingefunguka naye angejishindia heshima kuu.

⁴⁵ Mvulana mmoja mdogo, akiwa mwenye miguu myepesi sana, naye alijua vizuri sana kwamba angeweza kuwashinda mbio hao wavulana wengine kwenye hilo shindano, ama alidhani angeweza. Alifanya mazoezi siku baada ya siku, ya kukimbia. Aliyapampu mapafu yake madogo, akauzoeza mwili wake vilivyo, asije akachoka wakati akikimbia. Kisha akafanya mazoezi ya jinsi ya kuanza kwa miguu yake, na kuweza kuwatangulia hao wavulana wengine kwa mbali. Na jinsi ambavyo hana budi kupumua wakati akikimbia, kusudi apate kuishikilia oksijeni iliyoingia mwilini mwake, apate kuendelea kupampu, isije ikaukwamisha moyo wake kupita kiasi. Alijizoeza kutoka kila pembe aliyoweza.

⁴⁶ Basi kwenye ile asubuhi ambapo hizo mbio zilianza, kulikuwako na zaidi ya wavulana mia moja na hamsini wamepanga mstari, kwenye umri fulani. Mvulana huyu mdogo alikuwa kwa namna fulani mvulana mwenye kimo kizuri, kwa umri wake. Naye alikumbuka mazoezi yake yote. Basi

akajiandaa. Wakaingia mstarini, wakaweka maskini nyuso zao ndogo kwenye ka—kamba iliyokuja, wakasukumiza maskini pua yao dhidi yake. Alikuwa amesoma masharti yote ya hizo, akijiweka tayari.

⁴⁷ Ndipo bunduki ilipofyatuliwa, nao ule mstari ukavunjika, hao wavulana wadogo waliruka mbele. Basi maskini jamaa huyu mdogo alikuwa na mwili uliofanyiwa mazoezi vilivyo hata akaruka mbele ya hao wengine. Naye akakimbia kwenye barabara ya mbio kwa kasi sana, amefunzwa vizuri, hata angeweza kumshinda kila mvulana aliyekuwa kwenye mbio hizo. Naye alikuwa pale, loo, muda mrefu kweli, labda dakika moja ama zaidi, kabla ya aliye bora sana wa hao wakimbaji wengine kuwahi mahali pale.

⁴⁸ Lakini, katika mafunzo yake yote ya mwili, alikuwa amesahau lile neno la siri. Alikuwa amesahau jambo lile lile alilopaswa kusema, apate kuingia langoni. Naye akaenda huku na huku, na kuliwazia, akawaza na kuwazua niani mwake. Alikuwa amevutiwa sana na mambo ya kimwili, hali za kawaida za mwili wake, hata alikuwa amesahau jambo lililo muhimu. Huko, chini ya ule mstari, wavulana fulani ambao hawakukimbia mbio sana, walikumbuka lile neno la siri, nao wakaingia ndani.

⁴⁹ Ndivyo ilivyo siku hizi! Tumevutiwa sana na kujenga madhabahu makubwa, na makanisa na mijengo, na kadhalika, na tumevutiwa sana na kuyapamba makanisa yetu, kwa mijengo mizuri na mabenchi nadhifu ya kanisa na vinanda vizuri. Wahudumu wetu wamefunzwa vizuri sana kutoka... Wana digrii za Daktari DL., Ph.D., LL.D., bali tulisahau tunachokimbilia. Hiyo ndiyo shida. “Enendeni, mkawaambie wanafunzi Wangu ya kwamba nimefufuka katika wafu nami nitakutana nao huko Galilaya.” Tulisahau neno la msingi. Tumekuwa na shughuli nyingi sana na mambo mengine, kufanya makanisa makubwa, kujenga madhehebu makubwa, hata tukasahau lile neno la msingi.

⁵⁰ Maisha mengi yameokolewa kwa sababu ya maandalizi kwa ajili ya matukio yajayo. Wakati fulani uliopita, niliambiwa hivyo huko Florida, mwanahabari, taasisi ya hali ya hewa, ilituma habari ya kwamba dhoruba kubwa inakuja. Basi mtu mmoja alikuwa mfuga kuku, naye akamwendea jirani yake na kumwambia ya kwamba dhoruba ilikuwa inakuja. Akapuuza, na kusema, “Upuuzi!” Kisha akaendelea tu. Kamwe hakuweka kuku wake. Kamwe hakingia kwenye mtumbwi. Hakufanya matayarisho yoyote. Naye jirani yake alifanya maandalizi. Ila wote, yule aliyepuuza lile onyo, kuku wake wote, kuku wake wote walilipuliwa mbali na kuuawa, nyumba yake ikabomolewa, mali yake ikapotea, akapelekwa hospitalini. Yote kwa sababu hakujali wala kusikia onyo! Yeye alijua ujumbe ulitolewa, bali akakosa kuuti huo ujumbe.

⁵¹ Hivyo ndivyo imekuja siku hizi, kwa wengi wa watu wetu, kwa mengi ya makanisa yetu. Tunajua ya kwamba Biblia inafundisha ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tunajua ya kwamba Biblia inafundisha, Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, hata hivyo, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya; kazi kubwa kuliko hizi atazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba.” Sasa tumevutiwa na mambo mengine, pasipo kuchukua onyo, pasipo kujali. Tumekimbia, bali pasipo kutii Ujumbe. Tumeenda, ila hatukujua cha kuwaambia tukifika kule.

⁵² Siku chache zilizopita wakati makanisa ya ulimwengu huu, wakati makanisa ya Kikristo yalipoaibishwa na kutahayarishwa, wakati mheshimiwa na mtumishi mashuhuri mcha Mungu, Billy Graham, aliletwa uso kwa uso na Biblia. Alikuwa amekimbia, lakini alikuwa ameusahau Ujumbe; wakati Mwislamu yule alipomkabili uso kwa uso na kumwambia, “Iwapo hili ni Neno la Mungu, hebu tukuone ukilidhihirisha.” Alikuwa amekimbia vema, miamsho mikuu, mambo makuu. Lakini, ilipofikia mahali hapo, hakuwa na Ujumbe.

⁵³ “Nimefufuka katika wafu. Ni Mimi yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kukimbia kimwili, makanisa mazuri, wafuasi wengi, madhehebu makubwa, lakini hilo silo jambo la msingi. Angalieni kilichofuata, “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Akaenda, bali hakujua la kuwaambia.

⁵⁴ Mungu kamwe hakumtuma mtu pasipo kumpa jambo fulani la kusema. Mungu daima huthibitisha Maneno Yake.

⁵⁵ Kwenda, bali pasipo kuweza kuwaambia unapofika kule. Haidhuru miamsho yenu ni mikubwa jinsi gani, jinsi kanisa lenu lilivyo kubwa, ama jinsi dhehebu lenu linavyoyazidi hayo mengine, ikiwa hamna jambo la kuwaambia, mna kitu gani ila kundi la watu waliokusanyika pamoja kama chama?

⁵⁶ Tunao Ujumbe wa kuuambia ulimwengu, “Yesu yu hai! Yeye hajafa!” Kutii Ujumbe!

⁵⁷ Katika taifa hili kuu ambalo sasa tunatoa shukrani kwa ajili yake, Marekani, katika machafuko yake yote, katika upotovu wake wote, mambo yake yote mabaya, lingali ndilo taifa kuu kuliko yote ulimwenguni, na hapo mwanzo, kwa sababu lilianzishwa vizuri. Halijabeba Ujumbe.

⁵⁸ Miaka mingi iliyopita, wakati lilipokuwa katika uchanga wake, hadithi moja inanijia mawazoni mwangu, ya kwamba Waingereza walikuwa wakitaka kuchukua jumuiya ya taifa hili. Basi kulikuwako na kundi la watu lililokuwa limekusanyika na lilikuwa limeshika zamu, likifanya ulinzi. Ndipo kulikuwako na farasi aliyekuwa amefungiwa, na mwendeshaaji tayari kumpanda dakika yoyote. Jambo la kwanza alilopata ni ishara ya kwamba Waingereza walikuwa wakija, naye akamtagaa farasi wake. Ingemfaa nini kumwendesha kwa kasi farasi wake? Ingemfaa

nini kumpiga huyo farasi na kujaribu kuondoka kwenye kanisa hilo kwenda Boston? Ingemfaa nini kama hakuwa na ujumbe wa kuwaambia hao watu? Wangalijuaje kujiandaa?

⁵⁹ Akina Paul Revere wetu wa kisasa wamepiga mbio vizuri, bali, wanakimbia tu, hakuna Ujumbe. Saa imewadia, hali ya hatari inaendelea! Ulimwengu umefikia mwisho wake! Makanisa yamefikia upeo wao. Mataifa yamefikia upeo wao. Maisha ya mwanadamu yemefikia upeo wake. Sayansi imefikia upeo wake. Tumejiundia madhehebu na kufanya makanisa makubwa, tukawang'arisha wahubiri wetu kimwili na kuwaweka pamoja, hata wanajua jinsi ya kutumia vitenzi na vielezi vyao, na sauti zao na—na vokali zao zote, na kila kitu sawasawa kabisa katika saikolojia, kuwasiliana na watu. Bali hilo silo Yesu alilosema!

⁶⁰ “Katika Jina Langu watatoa pepo. Watanena kwa lugha mpya. Kama nyoka wa kufisha angewauma, asingewadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ulimwengu unahitaji mjumbe aliye na Ujumbe, kuwaambia jambo fulani, na kujua mahali huo Ujumbe unapotoka na umetoka kwa Nani.

⁶¹ Paul Revere, wakati alipompanda farasi wake, mtu shujaa, mtu aliye kwenye historia maadamu kuna taifa la kuwa historia yake. Alifanya usafiri huo maarufu kutoka kwenye vipandio vya hilo kanisa, akiwa na ujumbe uliomshtusha kila mtu, kuanzia kwa maskini hohehahe hadi kwa aliye tajiri kuliko wote, kuanzia kwa mkulima hadi kwa mfanyabiashara, “Waingereza wanakuja!” Ndipo wanamgambo wakajiandaa kwa ajili ya shambulizi. Nalo taifa hili kuu likaokolewa.

⁶² Kama urithi huu wa Mungu, kama watu hawa ambao Mungu aliwafia, kama Kanisa hili linaloitwa kwa Jina Lake, litaokolewa kamwe, hatuna budi kuwa na mjumbe aliye na Ujumbe kutoka kwenye kile Kiti cha Enzi, kukabiliana na changamoto ya siku hii. Kunaye Goliathi, bali Mungu hakika atakuwa na Daudi mahali fulani. Hatuna budi kukabiliana na mawasiliano. Hatuna budi kuwa na... Hatuna budi kuwa na Ujumbe.

⁶³ Tunaenda, ila hatuna la kusema. Inathibitika, tunapofika mahali ambapo taifa ama watu fulani wanaomkana Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu, na kusimama mbele ya wahudumu wetu walio na changamoto sana wa siku hizi. Halafu katika shirika letu kuu la kanisa, tunapata Wakomunisti thelathini wamebeba makaratasi kwa muda wa miaka ishirini ama thelathini, kwamba wao ni wafuasi wa chama cha Kikomunisti, katika makanisa yetu yaliyoungana. Tufanye nini? Inaonyesha ya kwamba wamekimbia bila Ujumbe; wakiuza haki zenyewe za urithi wa taifa, wakiuza haki za kawaida za urithi wa Kanisa.

⁶⁴ Yote yamefikia kwenye shindano la kuamua. Imefikia mahali ambapo lile Kanisa dogo ambalo limeamini Ujumbe, na kusimama kwa miguu yote miwili, huku macho yao yameelekezwa Msalabani, moyoni mwao ufufuo wa Yesu Kristo, unawaka moto! Imefikia mahali ambapo mataifa hayana budi kulitambua. Imefika kwenye onyesho la kuamua. Si ajabu kwamba makanisa. . . Wakati Baraza la Makanisa, limevamiwa sana na Ukomunisti, si ajabu hawawezi kuamini katika mambo ya kimbinguni. Si ajabu hawawezi kuamini katika uponyaji wa Kiungu; hawana Ujumbe wowote moyoni mwao, haidhuru wanakimbia kasi namna gani.

⁶⁵ Kama Roho Mtakatifu akiingia ndani ya moyo wa mtu, yeye ataamini ya kwamba Yesu Kristo amefufuka katika wafu, Naye yu hai ndani yake, kufanya, na kufanya mapenzi ambayo Yeye alikuja kufanya; mapenzi, mapenzi ya Mungu kupitia kwa maisha ya mwanadamu.

⁶⁶ Lakini, shida ni kwamba, tunakimbia, tunaondoka bila Ujumbe. Tunaenda pamoja na thiolojia. Tunaenda na namna fulani ya ufasiri wa kanisa wa Maandiko.

⁶⁷ Inatupasa kwenda na ule ufufuo! “Ati enendeni, mkawaambie wanafunzi Wangu ya kwamba nitaunda kanisa jipya”? La, bwana! “Enendeni, mkawaambie wanafunzi Wangu ya kwamba nimefufuka katika wafu, kama nilivyosema ningefufuka.” Huo ndio Ujumbe kwa Kanisa asubuhi ya leo, kwamba Yesu hajafa. Yu hai, na ni mkuu na mwenye nguvu tu leo kadiri alivyowahi kuwa.

⁶⁸ Tumekuwa na jumbe nyingi za ilani, kujitayarisha, Paul Revere na watu wengine wakuu, na vita vikuu na dhoruba, na kadhalika.

⁶⁹ Ndipo, Mungu hutuma Ujumbe wa faraja, pia. Huu ulikuwa ni Ujumbe wa faraja.

⁷⁰ Siku moja, walipokuwa na utumwa huko Kusini, Makaburu waliwaleta wenyeji huku kutoka Afrika Kusini, tunaowaita, siku hizi, “watu weusi.” Nao wakawaleta huku na kuwauza kwa Wamarekani huko Kusini, wakawafanya watumwa.

⁷¹ Maasi makubwa kulihusu huko Afrika siku hizi, mauaji ya kisiri, na kadhalika, yakiendelea. Wanapigania uhuru wao. Wanayo haki ya kuupigania. Mungu alimwumba mwanadamu; mwanadamu akawafanya watumwa. Kamwe halikukusudiwa.

⁷² Miaka michache iliyopita, nilikuwa kwenye uwanja mduara, ama jumba kuu la makumbusho, hasa. Nilikuwa nikitembea huko, nikiangalia picha mbalimbali na kadhalika, kwa kuwa napendezwa na sanaa. Nafikiri Mungu yuko kwenye sanaa. Ndipo nikapanda juu, nami nikaona kulikuwa na mzee Mnegro, alikuwa ni mkongwe sana, mabega yake yameinama, mzingo mdogo tu wa nywele nyuma ya kichwa chake. Alikuwa amevaa kofia yake. Naye alikuwa akitembea-tembea, na kitu fulani

kwa namna *hiyo*, akiangalia huku na huku, kana kwamba alikuwa akiangalia ama kutafuta kitu fulani kwenye jumba hilo la makumbusho. Nikasimama nyuma na kumtazama kwa muda kidogo.

⁷³ Basi baada ya kitambo kidogo akafikia kwenye kasha dogo pale. Ndipo akaangalia ndani yake, akagutuka, nayo macho yake yakaangaza. Akaruka nyuma kutoka kwenye hilo kasha kwa dakika moja, akavua kofia yake ndogo ya kizibo, akaishika mkononi mwake. Nikamtazama. Ndipo wakati maskini huyo mzee mweusi alipoinamisha kichwa chake, machozi yakaanza kudondoka kutoka mashavuni mwake. Nami nikamwangalia kwa mshangao, kwa kitambo kirefu kidogo.

⁷⁴ Ndipo nikawazia, “Nitachunguza kile kilichomsisimua sana maskini jamaa huyo.” Nikatembea nikazungukia upande *huu*, nayo ilionekana kwangu kama ni nguo iliyowekwa mle ndani.

⁷⁵ Basi nikamwangalia amesimama pale. Nami nikaenda hapo, nikasema, “Jambo, mjomba?”

Naye akasema, “Jambo, bwana.”

⁷⁶ Nami nikasema, “Mimi ni mhudumu. Nilishangaa kukuona ukiombea mahali hapa.” Nikasema, “Naamini kwamba wewe ni Mkristo.”

Akasema, “Naam, bwana.”

Nami nikasema, “Ni kitu gani kilichokusisimua sana?”

⁷⁷ Akasema, “Njoo hapa.” Nami nikatembea pamoja na huyo jamaa mkongwe, hapo. Akasema, “Unaona ile nguo?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Akasema, “Unaona doa lile lililo juu pale?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Kasema, “Hebu weka mkono wako ubavuni mwangu.”

Nikasema, “Mahali hapo panapoparuzi ni nini?”

⁷⁸ Akasema, “Mshipi wa utumwa ulipitia hapo, siku moja. Na *ile* ni damu ya Abraham Lincoln.” Akasema, “Damu yake iliundoa mshipi wa utumwa kwangu.” Kasema, “Je, hilo si lingekusisimua, pia?”

⁷⁹ Nikasimama hapo kwa mshangao. Nikawazia, “Kama damu ya Abraham Lincoln ingemsisimua—ingemsisimua mtumwa, kwa kumwondolea mshipi wa utumwa, Damu ya Yesu Kristo inapaswa kufanya nini kwa watu kama Rosella hapa, waliokuwa watumwa wa taathira ya ulevi; kwangu mimi, myonge mwenye mashaka, anayekufa?” Aliondoa mshipi wa utumwa wa dhambi moyoni mwangu. Hilo si linapaswa kumsisimua mtu? Si linapaswa kumfanya ajisikie tofauti? Si linapaswa kumfanya mwenye kicho anapoliwazia? Huwezi kuuona mti pasipo kukiinamisha kichwa chako, ni vigumu, ukijua ya kwamba Yesu aliyakomboa maisha yako juu ya Mti ule.

⁸⁰ Tunapoendelea, kwa muda kidogo, pamoja na watumwa, na wazo letu. Kulikuwako na matangazo, Ukombozi wa Kupiga Mbiu, uliotiwa saini, nao watumwa walikuwa wanaenda kuwa huru kwenye siku fulani. Hujui, loo, kama hujawahi kukutana na Kristo, kamwe hujui kile hilo lilimaanisha kwa hao watumwa. Wakati ulipotangazwa, ujumbe kote nchini, ya kwamba, “Mtakuwa huru kwenye siku fulani, wakati wa mapambazuko. Mtakuwa huru. Haitawabidi kuvaa mishipi ya utumwa tena, wala hamtapata kupigwa mijeledi tena. Bali mko huru, nanyi ni wenyeji wa taifa hili kuu la Marekani. Ninyi si watumwa tena, baada ya mapambazuko kwenye asubuhi fulani.” Loo, kwa matarajio makuu walingojea.

⁸¹ Laiti mwenye dhambi angaliweza tu kuona hilo! Laiti mwenye dhambi angaliisikia tu Injili ya kweli! Sio kujiunga na kanisa, bali kuhubiriwa kwa Injili, ya kwamba unaweza kuwa huru na dhambi, kwamba unaweza kuwa huru na maradhi yako. “Kwenye wakati fulani,” huo ni wakati utakapoamini.

⁸² Unajua, hao watumwa walisisimkwa sana na chini ya matarajio makubwa sana, wakiingojea ile sasa ambayo wangukuwa huru, mpaka, wananiambia, ya kwamba walikusanyika chini ya kilima kimoja, akina mama na watoto wadogo, wote walikusanyika, na baadhi ya wazee. Nao wakapanda hata juu ya hicho kilima, yapata usiku wa manane. Walijua itakapopambazuka na jua lichomoze, kwamba wangukuwa huru. Haitachukua zaidi ya nusu dakika jua kumulika kutoka juu ya kilima, lakini baadhi yao walikuwa juu ya kilima, wakiangalia, wakiangalia. “Loo, jua litakapochomoza, tuko huru.” Huyu alikuwa ni m-w-a-n-a [Kiingereza: s-o-n—Mf.] . . . ama, j-u-a [Kiingereza: s-u-n—Mf].

⁸³ Lakini wakati M-w-a-n-a atakapochomoza moja ya siku hizi! Na hapo M-w-a-n-a alipochomoza miaka elfu moja mia tisa iliyopita, Yeye alivunja kila mshipi wa utumwa, Yeye aliweka kila mateka huru, Yeye aliponya kila ugonjwa, aliwaweka huru hao walio kifungoni. Jinsi tunavyopaswa kupanda na kuangalia!

⁸⁴ Ndipo jua lilipopenyeza, kwanza, mtu aliyekuwa juu sana, akaliona, naye akampigia kelele mtu aliyefuata, “Tuko huru!” Naye mtu aliyefuata akampigia mtu aliyekuwa chini zaidi ya kilima, “Tuko huru!” Mpaka ikafika kambini, “Tuko huru!” Kwa kuwa, jua lilikuwa likichomoza, walikuwa wakingojea, wakingojea, wakiingojea saa hiyo.

⁸⁵ Ni zaidi sana vipi tunavyopaswa kuwa tuingojea, leo hii, M-w-a-n-a wa Mungu. Tuko huru na dhambi. Tuko huru na minyororo. Tuko huru na tabia. Tuko huru na kuvuta sigara, kunywa pombe, karamu za ulevi, kwa sababu M-w-a-n-a wa Mungu amefufuka kutoka kaburini na amevunja kila mnyororo. Hukumu zote zimekwisha! Deni imelipwa. Adhabu imelipiwa.

Dhambi zimeoshwa na kuondolewa mbali, nasi tuko huru. Loo, tuko huru, enyi watu! Utumwa? Uhuru, wakati Mwana wa Mungu anapozuka akiwa na uponyaji katika mbawa Zake!

⁸⁶ Siku moja Yeye atainuka kutoka kwenye Kiti cha Enzi, arudi duniani. Ndipo tutakuwa huru na uchungu wote na majaribu yote, huru na uchungu wote wa mwili na chochote kinachoambatana na maisha ya kimwili, kuishi pamoja na Yeye milele. Tutakuwa huru. “Enendeni, mkawaambie,” hilo ndilo jambo la kufanya.

⁸⁷ Katika wakati wa Biblia, kulikuwako na mwaka wa yubile uliokuja. Watu waliouzwa kwa sababu ya madeni waliyokuwa nayo, walikuwa na deni wala wasingeweza kuilipa, kwa hiyo walienda wakajiua kwa watu, kama watumwa. Nao ilibidi wawe mtumwa wao, mfungwa wao, maisha yao yote. Lakini, mara kwa mara, ilikuja siku ya neema, iliyojulikana kama mwaka wa yubile. Ndipo mwaka wa yubile ulipokuja, basi kuhani alitoka akapiga baragumu. Nayo baragumu hiyo ilionyesha kila mtumwa, haijalishi alikuwa ametumika kwa muda gani na ilibidi atumike muda gani zaidi, hapo baragumu hiyo ilipolia, mtumwa huyo aliwekwa huru. Angeweza kuweka chini jembe na kwenda nyumbani kwa watoto wake. Haikumbidi kufanya kazi muda mwingine zaidi, kwa sababu alikuwa huru hapo yubile ilipopigwa. Baragumu hiyo haikutoa sauti isiyojulikana, bali ilitoa sauti inayojulikana. Naye huyo mtu angeweza kuweka chini chombo chake, aende nyumbani akiwa huru na utumwa.

⁸⁸ Asubuhi ya leo, Biblia ilisema, “Na kama baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejua la kufanya?” Ikiwa Biblia imehubiri ya kwamba Yesu Kristo amefufuka katika wafu, Yeye ni yule yule jana, leo na hata milele, na baragumu tunazosikia zikipigwa siku hizi zinasema, “Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu,” ni nani watakaojua jinsi ya kujiandaa wenyewe?

⁸⁹ Tunachohitaji leo hii ni wajumbe waliopakwa mafuta kutoka kwa Mungu! “Amefufuka katika wafu! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele!” Huo ndio Ujumbe wa siku hizi.

⁹⁰ Loo, kumekuwako na jumbe kuu, bali Pasaka ilizitimiza zote! Jumbe kuu; Pasaka ilikuwa ni hizo zote! Wakati waliokufa...yalipofanywa matayarisho ya kwamba adui wa mwisho...Tulikuwa tumeyaona maradhi yakiponywa katika Agano la Kale. Tulikuwa tumeona miujiza ikifanywa katika Agano la Kale. Kulikuwa na maono yaliyokuja katika Agano la Kale. Lakini kila mtu alienda moja kwa moja kaburini, akishangaa kama atafufuka tena. Lakini kwenye ile asubuhi ya Pasaka, wakati hawa mitume walipopata Ujumbe ulio mkuu kuliko zote ambao mtu yeyote angeweza kupata, walipata kitu

gani? “Enendeni, mkawaambie wanafunzi Wangu, nimefufuka katika wafu!” Mauti yalikuwa yameshindwa!

⁹¹ Hakukuwa na mtu yeyote duniani, si nabii, si mtu mkuu, si mtu mtakatifu angaliweza kushinda... Wangeweza kushinda maradhi kwa Roho wa Mungu. Wangeweza kuushinda wakati, kwa Roho wa Mungu, na kuona kimbele mambo yaliyokuwa yakija. Wangeweza kushinda hilo. Lakini kamwe hapakuwapo na mtu aliyetiwa mafuta kwa upako kama huo kutoka kwa Mungu, ambaye angeweza kutoa tamshi hili, “Ninaweza kuyalaza maisha Yangu chini, nitayatwaa tena. Uvunjilie mbali mwili huu, nitaufufua kwenye siku ya tatu.” Kamwe hapakuwapo na mtu aliyeweza kutoa tamshi kama hilo. Nao walishangaa mioyoni mwao, kama hili lingekuwa ni kweli ama sivyo.

⁹² Lakini kwenye asubuhi ya Pasaka, walipata Ujumbe, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Nimefufuka katika wafu. Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: katika Jina Langu watatoa pepo; watanena kuwa lugha mpya; wakishika nyoka ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” *Ujumbe wa Pasaka*, ndio mmoja wa jumbe nzuri sana zilizopo. Mauti yalikuwa yameshindwa!

⁹³ Tunawazia juu ya mshindi. Napoleon, kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, alikuwa ameushinda ulimwengu. Aliushida ulimwengu, alilipiga kila taifa lililokuwako la kupigwa. Ndipo akakata tamaa sana kwa sababu hakukuwako na mtu mwingine wa kupigana naye, akaketi chini na kulia. Hapakuwapo na mtu mwingine yeyote wa kupigana naye, bali alitumikisha kanuni za huo mchezo vibaya. Makumi ya maelfu ya makahaba walilifuata jeshi lake, alienda na bunduki na upanga. Kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, alikuwa ameushinda ulimwengu. Lakini wakati mmoja yeye alikuwa mkataza pombe, naye akafa mlevi sugu hatari, kwa sababu alitumia vibaya kanuni za huo mchezo. Alikuwa ameusahau ujumbe. Alikuwa ameshinda, bali alikuwa ameusahau ujumbe. Alienda, bali alisahau kile alichokuwa akienda.

⁹⁴ Kama yule mvulana mdogo aliyezikimbia zile mbio, kama kanisa linavyokimbia siku hizi, kama wale watu wanaokimbia, kama taifa linavyokimbia! Kimbilio letu si mabomu ya atomiki, kimbilio letu ni Yesu Kristo na kufufuka Kwake.

⁹⁵ Napoleon alikuwa amesahau jambo la msingi. Alipatwa na nini? Alikufa ameshindwa kabisa, mlevi sugu. Kwa nini? Yeye hakufuata kanuni za huo mchezo vizuri, ingawa alikuwa ameushinda ulimwengu, kimwili. Alikuwa amelitayarisha jeshi. Alikuwa bingwa wa kijeshi, aliliteka kila taifa na kufanya

hayo mambo (ambayo yeye) ambayo hakuna mtu mwingine angaliweza kufanya ama hata aliyepata kuyafanya, kama yeye, ila alikuwa amesahau kwamba ujumbe halisi ulikuwa ni upi. Alikuwa ameuteka, na kupata nguvu zake za kijeshi, bali alisahau nguvu za Bwana.

⁹⁶ Nguvu za Bwana ndizo faraja yetu. Hatuna nguvu zingine. Sina kimbilio lingine, hata moja! Mungu uturehemu! Yachukue maisha yangu, bali kamwe usiniache nisahau mahali zitokapo nguvu zangu. Zinatoka kwa Bwana! Sitaki mambo mazuri ya ulimwengu. Ninamtaka Yesu, ninataka ufufuo Wake ukiwaka maishani mwangu.

⁹⁷ Hiyo ilikuwa tofauti jinsi gani na Yesu Kristo kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu! Kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, Yesu alimiliki kila kitu; Yeye aliuumba ulimwengu. Naye alikuwa katika ulimwengu, wala ulimwengu haukumtambua. Hakujifanya kama ana utukufu. Hakukusanya mwanajeshi yeyote. Kamwe hakuundia madhehebu makanisa yoyote. Kamwe hakujifanyia Mwenyewe majina yoyote makuu. Kamwe hakujitokeza na digrii zozote za kujivunia za fundisho, thiolojia, na kadhalika, kamwe hapakuwapo na kumbukumbu Yake akienda kwenye shule yoyote ya thiolojia. Ila alikuwa na Mungu. Alikuwa na Mungu. Na kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, Yeye alikuwa ameshinda kila ibilisi aliyekitokeza kichwa chake katika kuzimu. Alishinda maradhi. Alishinda ushirikina. Alishinda ibilisi. Alikuwa ameyashinda mauti. Ndipo alipokufa Msalabani, alishuka katika mashimo yasiyo na mwisho ya kuzimu, na kuishinda kuzimu.

⁹⁸ Ndipo kwenye asubuhi ya Pasaka akalishinda kaburi. Kwa nini? Yeye alitumia kanuni za mchezo vizuri, akikimbia na Ujumbe. Alikuwa, aliondoka! “Nenda.” Mungu alimtuma, Naye alikuwa na Ujumbe wa kuwaambia. Basi pamoja na Ujumbe ambao Mungu alimpa, Yeye alishinda nguvu za Shetani. Alishinda maradhi. Alishinda mauti. Alishinda kuzimu. Alishinda kaburi. Kwa nini? Alienda! “Enendeni, mkawaambie!” “Sikuzote nafanya yale Baba Yangu anionyeshayo kufanya. Sifanyi neno ila lile Yeye aniambialo nifanye.”

⁹⁹ Ndipo kabla hajafa, Yeye alisema hivi, “Kama vile Baba alivyoniipeleka, nami nawapeleka.” Sio kuwajenga watu kwa nguvu za kijeshi; sio kuweka wakati wako wote juu ya ni nani atakayekuwa Rais. Huenda hilo likawa ni muhimu, bali si muhimu katika *Hili*. Ulimwengu huu umekwisha. Tunao Ujumbe mmoja, huo ni, Yesu Kristo alifufuka katika wafu, Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁰⁰ Jana, katika chumba kidogo cha mahakama, walikuwa wakijaribu kunifanya niseme jambo ambalo halikuwa sahihi.

Nikasema, “Mimi si jambazi.” Nikasema, “Mimi—mimi—mimi ni mwaminifu. Wala huwezi kusema zaidi ila yaliyo kweli.”

¹⁰¹ Basi mtu fulani alikuwa pamoja nami, kasema, “Kama mtu angezungumza nami namna hiyo, ningejisikia kumtupia kitabu.”

¹⁰² Nikasema, “La, bwana. La, hilo si sawa. Hiyo siyo njia ya kuliendea. Si sawa.”

¹⁰³ Akasema, “Vema, mbona hujui mambo haya huendelea? Kwa nini wewe huko huko nje ukifanya jambo hili?”

Nikasema, “Ninatumia wakati wangu kumtumikia Yesu Kristo.”

¹⁰⁴ Ee Mungu, loo, watu ni vipofu wala hawawezi kuliona! “Kama vile Baba alivyonipeleka,” Baba alimpeleka, Yeye akaenda. Alikuwa na Ujumbe wa kuwaambia watu. Na kwenye ile saa ya mauti, Yeye alishinda mauti na kushinda kuzimu, na kushinda kaburi. “Kama vile Baba alivyonituma na Ujumbe, ninawatuma na Ujumbe; sio kujenga makanisa, madhehebu, bali enendeni ulimwenguni kote mkadhihirishe Nguvu za Roho Mtakatifu. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya, watashika nyoka.” Na wakati miili yetu ikiingia kaburini, kama Wake ulivyofanya, Yeye ameshinda mauti, kuzimu, na kaburi. Yeye ni Mshindi mkuu.

¹⁰⁵ Yeye hututuma na Ujumbe Wake. Hebu twende pamoja na Ujumbe, twende na kitu cha kuwaambia. “Enendeni, mkawaambia!” Sio kukimbia halafu msiweze kuwaambia, hebu kwanza tuuingize moyoni mwetu wenyewe.

¹⁰⁶ Unapokuja kuombewa, asubuhi ya leo, usije bila mpango. Njoo ukiwa na Ujumbe moyoni mwako, “Mimi Ndiye niliyekuwa nimekufa, na ni hai tena. Mimi Ndimi niliyewapa Ujumbe, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.’” Kama Mungu Mwenyezi angeweza kumchukua ma—maskini mtoto mchanga mwenye makengeza na kuyafanya macho yake kawaida tena; Mungu angeweza kumchukua mtoto mchanga, mtoto mvulana azaliwe, hakuwa amewahi kuona maishani mwake, na mwenye umri wa miaka kumi na sita, ayafungue macho yake tena; Mungu anaweza kumfanya mtu mnyonge aliyeliwa na kansa . . .

¹⁰⁷ Na kwa sababu Ujumbe ni wa kweli, kwa sababu Mungu alituma Ujumbe, kwa sababu Mungu alituma mjumbe, hapana shaka kwamba kila bunduki ya kuzimu itakuwa ikimrushia risasi. Hiyo ni kweli, atajikwaa na kuanguka, na kusimama na kutikisa kichwa chake, na kuendelea. Tunao Ujumbe, hakuna kitu kitakachoukomesha! Haleluya! “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayatalishinda.” Wanaweza kusema watakayo, wafanye watakayo, ibilisi anaweza kughadhabika na kulia vikali. Lakini Yesu alifufuka katika wafu, Yeye anaishi leo ndani yetu!

¹⁰⁸ Siku chache zilizopita, nikizungumza na yule Daktari mkuu Lamsa, ambaye aliitafsiri Biblia kutoka kwenye Kiaramu, hadi Kiingereza. Nami niliona ile ishara ndogo, ishara ya Mungu pale juu, pamoja na nukta tatu ndogo ndani yake. Nikasema, “Daktari Lamsa, nini hicho?”

Akasema, “Ni Mungu, mwenye sifa tatu.”

¹⁰⁹ Ndipo nikasema, “Unamaanisha, Mungu akiishi katika ofisi tatu, kama vile, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?”

¹¹⁰ Akasimama na kuniangalia, machozi yakaingia kwenye macho ya Myahudi huyo, akasema, “Unaamini hilo, Ndugu Branham?”

Nikasema, “Kwa yote yaliyo ndani ya moyo wangu.”

¹¹¹ Akanikumbatia, na kusema, “Nilishangaa wakati nilipoona kule mambo makuu yakiendelea, na ishara ambazo ulikuwa ukifanya.” Kasema kwamba, “Waliniambia wewe ulikuwa nabii. Sikuamini hilo, mpaka sasa. Sasa ninajua ndivyo ulivyo.” Akasema, “Hiyo ni kweli! Huo ndio Ujumbe. Hilo ndilo jambo litakaloutikisa Ufalme wa Mungu.” Naam. Akasema, “Siku muhuj utakufa kwa ajili yake, jamani.” Kasema, “Utatia muhuri ushuhuda wako kwa jambo lilo hilo.”

¹¹² Mmoja wa watu wakuu sana tulio nao, wakati Eisenhower na watu mashuhuri wa ulimwengu, Hollywood, kila namna ya mabingwa wa sinema na kila kitu kikimwita, lakini alikaa moja kwa moja mkutanoni. Akasema, “Nimetumia miaka thelathini na kitu, nikifanya tafsiri hii, sio kutoka kwenye Kiyunani cha Vatikani, bali kutoka kwa Kiaramu; moja kwa moja kutoka kwenye hicho, kutoka kwa Kiaramu, hadi Kiingereza.” Kisha akasema, “Nimetumia wakati huo wote,” akasema, “sasa hivi ndiyo nimefikia mahali ambapo nimemwona Mungu wa Biblia, akitenda kazi.” Akasema, “Unajua, Ndugu Branham, tunaweza kuona ishara na maajabu, bali tunachunguza hiyo ishara ina Sauti gani. Sisi Wayahudi, tunaona ishara, bali tunachunguza Sauti ya hiyo ishara.”

¹¹³ Loo, haleluya! Sauti ya ishara! Mungu alimwambia Musa, “Wasipoisikia hiyo Sauti, Sauti ya ishara ya kwanza, basi watasikia Sauti ya ishara ya pili.” Si sana sana ile ishara, bali Sauti iliyoambatana nayo.

¹¹⁴ Mnaona, Myahudi huyo, yeye alijua alilokuwa akizungumzia. Akasema, “Nimeona upambanuzi, nimeona ishara, maajabu, vipofu wakiponywa, na namna zote za ishara mbalimbali, bali nikashangaa, bali sasa ninaiona Sauti iliyo nyuma yake hutamkata Mungu katika vipande vitatu, na kusema, ‘Yeye ni Mungu mmoja, Baba, na wa pili, Mwana, . . .’ Yeye anasema, ‘Mungu ni Mungu: sifa tatu za Mungu; ofisi tatu za Mungu.’” Kasema, “Hilo linalithibitisha.”

115 Loo, ndugu, tunao Ujumbe! “Enendeni, mkawaambie wanafunzi Wangu! Sikuwa *mmoja* aliyekufa, na *mwingine* karibu sana na kufa, na huyo *mwingine* yu hai. Mimi ni Yule Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja; Shina na Mzao wa Daudi; Nyota ya Asubuhi Ing’ayao.” Naam!

116 Inafaa nini kwenda, nini kwenda, ikiwa huna kitu cha kuwaambia? Tuna kitu cha kuwaambia, hiyo ni kweli: “Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, anawapenda nyote. Aliwafia ninyi nyote. Mpendeni Yesu Kristo Mwana wa Mungu.”

117 Ni wangapi wamewahi kuwa mikutanoni, na kuziona ishara kuu na maajabu ya kuonekana Kwa—Kwake, jinsi Yeye anavyotambua na kuonyesha, na kadhalika? Huyu ni Mungu wa Mbinguni, Yule ambaye amefufuka katika wafu.

118 Mnapaswa kuona ishara ya ishara Yake ya Kiebrania. Ni Nuru, kama Nguzo ya Moto, na mle ndani mna alama tatu ndogo, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ambao hawakuwa ni watu watatu. Ilikuwa ni Mungu mmoja akiishi katika ofisi tatu. Mungu yule yule! Haleluya! Mungu juu yenu, Mungu pamoja nanyi, Mungu ndani yenu. Yeye yule akijidhili Mwenyewe, akilisafisha Kanisa Lake, apate kuishi. Unapomkatakata vipande-vipande, na kumweka mmoja *hapa* nje, na mmoja *hapa*, mmoja *pale*, ni upagani mtupu.

119 Ninaamini kule kufufuka kwa Yesu Kristo, aliyefufuka katika wafu. Naye Ndiye Mtu pekee angaliweza kusema ya kwamba, “Mamlaka yote Mbinguni na duniani yamewekwa mkononi Mwangu. Mamlaka yote Mbinguni na duniani yamewekwa mkononi Mwangu. Enendeni ulimwenguni kote, mkahubiri Injili kwa kila kiumbe.” Injili ilikuja si kwa neno pekee, bali kwa nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu. Mungu akusaidie kuamini hilo, Mungu anisaidie kuamini hilo, nasi tutamwona Yesu siku moja.

Wakati masumbuko ya maisha
yatakapokwisha, tutamwona Yesu hatimaye;
Juu ya Kiti Chake cha Enzi cha kupendeza,
atanikaribisha Nyumbani,
Baada ya siku kwisha. (Hiyo ni kweli.)

Changarawe zimefagiliwa katika nyayo za
miguu
Za yule Mgeni kutoka pwani ya Galilaya.

120 Walimwua kwa sababu Yeye alijifanya Mwenyewe Mungu, Naye alikuwa ni Mungu. Walimtundika, kwa sababu, Yeye alikufa chini ya adhabu ya kifo. Hiyo ndiyo sababu siamini katika adhabu ya kifo. Yesu alikufa chini ya a—adhabu ya kifo kutoka kwa serikali ya shirikisho la Urumi. Adhabu ya kifo, ilikuwa, kutundikwa msalabani. Alikufa chini ya adhabu ya kifo, wakamvua nguo Zake, naye akaning’inia pale,

wakamwaibisha, Naye akafa chini ya hali hiyo. Bali Mungu akamfufua kwenye siku ya tatu!

¹²¹ Nasi ni mashahidi Wake. Basi tusipomtetea, ni nani atakayemtetea?

¹²² Mtu mmoja alikutana nami hivi majuzi, kasema, “Loo, Ndugu Branham, usiwaambie. Acha kuwaambia. Una—unaziudhi hisia za wanawake, kuhusu wao kukata nywele zao, na kuhusu wao kufanya *hivi* na kufanya *vile*, na kadhalika namna hiyo.”

¹²³ Nikasema, “Kama nisipowaambia, ni nani atakayewaambia? Ni nani atakayeyatangaza?”

Kasema, “Vema, unawakasirisha hao wahubiri.”

¹²⁴ Afadhali wanikasirikie mimi, kuliko Yeye. Ni Kweli. Hiyo ni kweli! [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kweli. Ni nani atakayeyatangaza? Mtu fulani hana budi kuyatangaza.

¹²⁵ Yesu alisema, “Enendeni, mkawaambie. Nendeni na kuwaambia, mkawaambie wanafunzi Wangu ya kwamba nimefufuka katika wafu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari.”

¹²⁶ Mnaamini hilo, enyi marafiki?

Na tuombe, tunapoviinamisha vichwa vyetu sasa kwa maombi.

¹²⁷ Ee Baba Mungu! Hakika, “Enendeni, mkawaambie. Enendeni, mkawaambie wanafunzi Wangu ya kwamba nimefufuka katika wafu.” Na Baba Mungu, si kwamba tu uliwaambia wanafunzi Wako, bali uliwathibitishia ulifufuka katika wafu. Ulijionyesha Mwenywe pamoja nao, na kufanya yale hasa uliyofanya kabla hujafa. Miaka elfu moja na mia tisa imekuja na kwenda, Bwana, Ujumbe ungali unawaka moto. Ni angavu tu na unawaka moto mioyoni mwetu leo hii kama ulivyokuwa kwa hao wanafunzi, kwa kuwa tunamwona Bwana aliyefufuka moja kwa moja miongoni mwetu, akifanya mambo yale yale aliyofanya hapo awali. Tunajua ya kwamba amefufuka katika wafu.

¹²⁸ Pasaka inamaanisha mengi kwetu, kwa sababu tumejiunga na tunafurahia ushirika wa kufufuka Kwake. Kwa kuwa wakati mmoja tulikuwa tumekufa katika dhambi na makosa, kama yule mwana mpotevu, lakini sasa tumepata neema, na Mungu ametusamehe dhambi zetu. Pia ametupatia Muhuri, kama alimvyomfanyia Baba Ibrahimu, kuthibitisha kwamba Yeye ametukubali. Baba Ibrahimu alisema alimwamini Mungu, bali akampa muhuri wa tohara kama thibitisho ya kwamba yeye kweli alimwamini. Na sasa, Baba, leo hii sisi tumetahiriwa kwa Roho Mtakatifu, mambo yote ya ulimwengu yamepita. Tuna lengo moja: kukutumikia Wewe. Tuna shauku moja: kukupenda Wewe, kuwa mwanafunzi Wako.

¹²⁹ Na sasa, Bwana, naomba ya kwamba Wewe utauthibitisha maskini ujumbe huu uliovunjikavunjika kwa kila moyo. Jalia wasiukose. Jalia waone ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ya kwamba uko hapa, umefufuka katika wafu, na utakuwa mpaka Ro—Roho na mwili zitakapoungana pamoja tena kwenye kule Kuja Mara ya Pili.

¹³⁰ Ninawaomba wagonjwa walio hapa, Baba, asubuhi ya leo. Sasa, kwenye asubuhi hii ya Pasaka, nimeweka kando (ama, sio kuweka kando, bali kuweka karibu kwa muda kidogo) zile karama ambazo Wewe umenipa, kama vile upambanuzi. Ulimwengu, nimekuwa huku na huku kote katika mataifa, Bwana, wote wanajua hilo. Sasa ninaomba, ya kwamba, ule Ujumbe ambao Wewe ulinipa hapa juu mwituni, kwamba, siku chache zilizopita, ya kwamba, juu ya zile nguvu za uumbaji zilizo kwenye kanisa hili asubuhi ya leo, wale watu wenyewe zilizoumbiwa, ninaomba, Mungu, wakati nikija kuweka mikono yangu juu wa wagonjwa asubuhi ya leo, pamoja na ndugu zangu hapa, ya kwamba utaliangukia kanisa hili asubuhi ya leo, kwa rehema, na kwamba utawaponya hawa watu, hata hapatakuwa na mtu mmoja mnyonge miongoni mwetu wakati ibada itakapokwisha. Jalia kila mmoja wao abarikiwe na aponywe.

¹³¹ Tunatambua, Bwana, si kitu ambacho tungeweza kujiingiza wenyewe kwacho. Ni imani rahisi kama ya mtoto, kuamini. Tunaweza kuwaona wale wanafunzi wakiisha kupewa nguvu za kuwaponya wagonjwa, waliondoka nao wakashindwa penye ugonjwa wa kifafa; wakipiga mayowe na kulia, labda, na kurukaruka juu chini, na kujaribu kumfanya ibilisi huyo aondoke. Lakini wakati alipokutana na Yesu, loo, ni tofauti jinsi gani! Yeye alisema, “Ewe pepo mchafu, toka ndani yake.” Ni tofauti jinsi gani! Loo, alijua ya kwamba huyo hakuwa ni mtume. Huyo alikuwa ni Bwana Mwenyewe. Naye huyo pepo akamrarua huyo mvulana na kumtupa chini. Lakini Yesu alisema, “Hajafa. Mchukueni tu mkampe chakula.” Huyo pepo mchafu alikuwa ameondoka.

¹³² Ee Yesu, Ewe Mwana wa Mungu, njoo tena, litie mafuta Kanisa Lako bure, kabisa, kwa nguvu. Jalia Roho wa Yesu aliye hai aliyefufuka alifufue maskini kanisa hili dogo asubuhi ya leo katika imani mpya, nguvu, nguvu za imani, tupate kumwaibisha kila mwenye kupinga. Tujalie, Bwana. Tunawakabidhi watu hawa wote Kwako, tukiomba ya kwamba utawabariki na kuwapa wokovu kwa nafsi zao, uponyaji kwa miili yao, kupitia kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

¹³³ Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, nitaauliza swali. Kunaye mtu hapa asiye Mkristo, angetaka kukumbukwa sasa, na kusema, “Uniombee, Ndugu Branham”? Mungu akubariki hapo. Mtu mwingine, “Mimi si Mkristo. Nimesikia habari kwamba Yesu alifufuka katika wafu, bali kweli sijui hilo. Yeye kamwe

hajafufuka moyoni mwangu. Sina ridhaa. Mimi ni mgonjwa, pia. Nitapita kwenye mstari wa maombi, nirudi na kupitia mwingine, nirudi na kupitia mwingine. Nitaenda kutoka kanisa moja hadi lingine, na mahali hadi mahali.” Hilo silo. Ni kumwamini Yeye. Yeye amefufuka katika wafu. Hilo latosha. Mtu mwingine ungeweza kuinua mkono wako? Useme. . . Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mtu mwingine, “Nataka kuamini. Nataka kuamini”?

¹³⁴ Ni wangapi walio wagonjwa hapa ndani? Inua mkono wako, useme, “Nataka kuamini. Nataka kuujuu Ujumbe asubuhi ya leo.” Mungu awabariki. Hilo ni zuri. Naam, Mungu akubariki, mwanangu. Vema. Sawa.

¹³⁵ Sasa, Teddy, ninakutaka ucheze “*Tabibu Mkuu*,” kwa dakika moja, tafadhali, “sasa yu karibu.” Ndipo wakati unapofanya hivyo. . .

¹³⁶ Hilo ni gumu sasa hivi. Maono yanatokea kote jengoni, mnaona. Naam, ninajaribu kuninii, nilikuwa nikijaribu kuifanya hii kuwa ni ufufuo, wa juu zaidi wa juu zaidi kutoka kwenye—kutoka kwenye lundo la majivu ninakolazimika kuketi. Ninataka ufunuo zaidi kidogo. Ninajua jambo moja: maadamu ninashikilia hiyo huduma ya kwanza, ya pili haitakuja, haikuja. Sasa maadamu ninashikilia ya pili, ya tatu haitakuja, mnaona. Inanibidi kutoka moja kwa moja, kutoka nje na kuiamini, “Mungu alisema hivyo!” Siku chache zilizopita. . .

¹³⁷ Sasa mnaweza kuviinua vichwa vyenu sasa mkitaka. Ninayo mikono yenu; Mungu anayo.

¹³⁸ Nataka kuwaambieni kitu fulani kidogo. Ndugu Ed Daulton, ninaamini ndiyo kwanza aingie mlangoni, ndugu mzuri wa Kibaptisti, yeye pamoja na mkewe. Ndugu Jeffries yuko hapa mahali fulani. Othel Jeffries. Naye yuko hapa, ninajua yuko hapa mahali fulani. Hata hivyo, hao ndugu walikuwa wamefanya mkutano nipate kwenda, huko chini Kentucky. Ndugu, ndugu wa thamani, wakiupenda ujirani wao na watu wao. Wakapata majumba ya mikutano na maghala ya silaha na kadhalika, kwa ajili ya ibada ya usiku mmoja tu, walikuwa wamekodi maghala ya silaha. Maskini J. T. Hoover, lolote lile. . . L. G. Hoover alikuwa ameutengeneza mmoja huko chini Elizabethtown. Naye Ndugu Ed Daulton huko Willow Shade ama—ama Somerset, Somerset. Na ndugu, huyo ndugu mwingine alikuwa huko chini karibu na Glasgow, mahali nilipozaliwa. Watu huko ndani ambako nilizaliwa na kulelewa, ambako Malaika wa Bwana alinitokea kwa mara ya kwanza.

¹³⁹ Nami nilitaka kurudi. Lakini nikasikia mguso mdogo. Nami nikasema, “Vema, kwa ajili ya hao ndugu, nitaufanya huo mkutano.” Mara nilipofika kwenye bonde hili, koo langu likafungika kabisa wala sikuongea kwa siku tisa, mpaka mikutano hiyo ikapita.

¹⁴⁰ Ndugu Ruddell, huenda akawa hapa asubuhi ya leo, pia, mmoja wa ndugu kutoka maskani hii, yeye pamoja na Junie Jackson na hao wengine, nilikusudiwa kumfanyia mkutano. Na mara, koo langu likafungika tu. Basi muda si muda mwajua, nikashikwa na homa ya karibu mia moja na tano. Nami nilikuwa nikienda mkutanoni, kwanza, naye—naye Doc Schoen akaniambia. . . Nikasema, “Nimepwelewa na sauti.”

¹⁴¹ Akasema, “Nitakupa kitu fulani kulegeza zoloto, ndipo uendelee na kuhubiri.” Nami nikameza kitu fulani alichonipa, na, kile kilichokuwa, kiliuvuta uwazi huo chini na kuufunga. Ndipo nikalala kitandani kwa muda wa siku tisa, nikiwa tu na homa kali mno.

¹⁴² Wengi wa ndugu zangu hapa walinijia, ndugu wengi mashuhuri walikuja wakaniombea. Hapa akaja Ndugu Graham Snelling, hapa akaja Ndugu Ruddell, ndugu hawa wote hapa, wote wakakusanyika, wakiomba na kadhalika. Mimi nikiomba, nikijaribu niwezavyo, hata nisingeweza kunong’oneza. Nikashangaa, “Yote haya yanahusu nini?” Maskini mke wangu mpendwa ameketi pale, yeye na hao wengine wakiniombea, nikaendelea tu kukaa vile vile. Wasingeweza kuelewa.

¹⁴³ Sasa, yeye alinipa dawa za kunywa, bali sikuzinywa, kwa sababu zilikuwa ni za kulevya. Ndipo basi nikaachilia tu. Nami nikaendelea tu kuwazia, “Bwana, hakika!”

¹⁴⁴ Halafu basi, baada ya hiyo mikutano kwisha kabisa, Jumatatu (hiyo ilikuwa, mkutano wa mwisho, ulipaswa kuwa Jumamosi), na halafu (ninaamini), halafu basi, Jumatatu nilikuwa nimejaribu kuamka. Nilikuwa dhaifu sana, nisingeweza kupitia chumbani. Nikaketi.

¹⁴⁵ Mwajua, ninashukuru sana kwa ajili ya mke aliyetolewa na Mungu. Nanyi je, ndugu? Mke halisi, mwenza halisi!

¹⁴⁶ Nikaketi chini. Nikamwashiria, na kumleta karibu nami. Nami nikasema, “Meda, wakati mwingine nashangaa,” nikasema, “nashangaa, kuna nini.” Nikasema, “Kwa nini hiyo mikutano iwe pale, na Mungu aniache nilale namna hii?” Nikasema, “Ni kwa nini?” Kisha nikasema, “Wakati mwingine mimi hushangaa kama kweli Yeye aliniita.”

¹⁴⁷ Akasema, “Kwani hujionei aibu?” Mnaona? Naye akaniambia, kasema, “Bill, hujui kwamba Mungu anajua kile anachofanya nawe? Tulia, tulia tu.”

¹⁴⁸ Na kwa hiyo nikaingia. Hilo kwa namna fulani lilinikemea, mwajua. Na kwa hiyo nikaingia na kulala kitandani. Akaja kubadilisha mashuka. Naye alikuwa amechukua hivyo—hivyo vitu mkononi mwake, ndipo alipoanza kutoka, nikaangalia, na kulikuwako na . . .

¹⁴⁹ Nikaona maski-. . . jengo kubwa mno la ghala la silaha, ambalo jua lilikuwa limemulikia na kulipuka chini, kulilipua

vipande-vipande, jua likiwaka kutoka Mbinguni. Ndipo pakatokea wanawake watatu pamoja na mwanamume mmoja, wakaja. Nao walikuwa na vitu vidogo, kama ninii ndogo... namna fulani ya bunduki za kupiga risasi, kitu kama hicho. Naye akasema, “Hiyo hupigilia misumari.” Kisha kasema, “Tutaninii... Wewe inua vipande hivi juu, Ndugu Branham, nasi tutakujengea ghala hili la silaha tena.”

Nami nikasema, “Vema, nitafanya hivyo.”

¹⁵⁰ Lakini kitu Fulani kikasema, “Usifanye hivyo.” Vema, nikaunyosha mkono kuchukua kipande kimoja, namna *hii*, kulijenga namna *hii*. Na papo hapo Sauti ikanena nami, na kusema, “Sasa wako njiani kukufanya urudi. Usiamini hilo.” Kasema, “Wao daima ni waaminifu sana, nao wanakuja kwako wakiwa na BWANA ASEMA HIVI, ila wamekosea.” Mnaona?

¹⁵¹ Fred Sothmann, wengi wao hapa, walikuwa pale pale nilipowaambia kuhusu jambo hilo. Chini ya saa moja, hao watu wakaja kwa gari hadi mlangoni pangu. Nikasema, “Wale pale wanawake watatu na mwanamume mmoja.”

“Hiyo ni kweli kabisa.”

“Wanakuja wakiwa na BWANA ASEMA HIVI?”

“Naam, bwana, wao... ”

¹⁵² Nikasema, “Bila shaka, mnajua la kuwaambia.” Wamekosea wangali wanyofu, mnaona. Watu wazuri, bali wamekosea wangali wanyofu. Mnaona?

¹⁵³ Ndipo nikawazia, “Vema, nifanye nini? Nifanyeje?” Ndipo Meda akaingia, naye alikuwa amerudi nyuma. Naye Ndugu Freddie akaenda na kuwaambia hao watu. Ndipo baada ya kitambo kidogo, nilikuwa mle ndani ki-kitandani, nami nikawazia, “Kwa nini itukie hivyo? Kwa nini siwezi kuzungumza? Kwa nini siwezi kuzungumza na mtu fulani, ama chochote kile?” Nami nilikuwa nimelala mle ndani. Ndipo Meda akaingia, naye alikuwa akitoka chumbani.

¹⁵⁴ Ndipo nikaangalia, nami nikaona kitu fulani kikimemeteka upande mmoja. Basi nikaangalia, na kulikuwako na huu... ukuta wangu ukafunguka, ndipo nikamwona Yesu. Ni wangapi wenu waliopata kunisikia nikisema ya kwamba nimemwona Yesu mara mbili maishani mwangu, katika ono? Nami niliamini nitamwona tena kabla ya wakati wa mwisho, mnaona, kumwona tena. Sasa, nikaangalia, nazo anga zilikuwa moja kwa moja huko nje, ilionekana tu kana kwamba nilitazama kupitia ukutani. Basi kulikuwako na Biblia imesimama moja kwa moja namna *hii*, Biblia kubwa mno imesimama angani. Vema, kuna kitu fulani kilichotia nuru kuizunguka hiyo Biblia, na kutoka kwenye Biblia ukaja msalaba mzuri sana wa dhahabu. Nao ukasimama namna *hii*, nazo nuru zikitoka pande zake zote, na kutoka kwenye msalaba huo Yeye akatokea. Hiyo Biblia iliukisi huo

msalaba, nao msalaba ukamwakisi Yeye. Akaja akitembea, akaja papo hapo nilipokuwa. Ninaweza kumwona dhahiri, ninaweza kuuona huo msalaba ukiziakisi nywele Zake akisimama pale, zikining'inia juu ya uso Wake.

155 Akaniangalia chini namna *hiyo*, Naye akaniambia, “Unangojea uthibitishiwe huduma yako mpya.” Akasema, “Tayari nimekuthibitishia. Imethibitishwa tayari. Huna budi kuikubali.” Mnaona? Nami nikasimama na kumsikiliza kwa dakika moja tu. Ndipo nikakumbuka. Sikusikia hilo, liliingia tu niani mwangu.

156 Kama vile mtu ambaye amekuwa mwenye dhambi maishani mwake mwote, naye anajua kuna Biblia, anajua kuna Mungu, bali mara moja anasikia mahubiri, kisha kitu Fulani kinamwambia, “Ni wewe.” Ndipo, Neno lilo hilo limekuwa hapo wakati wote, hata hivyo linathibitishwa kwake, ndipo anasema, “Bwana, nisamehe.” Ila haitafaa kitu mpaka anapoukubali wokovu wake, ndipo anatoka nje naye ni Mkristo. Haidhuru analia jinsi gani, anasihi jinsi gani, hana budi kuukubali Huo.

157 Naye akaniambia basi, “Huna budi kuikubali vile vile. Huna budi kuiamini.”

158 Mimi naogopa kushindwa. Chochote kile, ninahofia nitaleta aibu. Sikuzote ninahofia hilo, nikiangalia, ninafikiri nitaita kitu kingine. Maana, nimechukua maonyo ya Biblia, jinsi ambavyo Musa alipewa nguvu kuu, naye akaupiga mwamba badala ya kusema nao. Ninamkumbuka Eliya, kwa kuwa alikuwa kipara, hao watoto wadogo wakimtania kuhusu kuwa na kipara; basi akaweka laana juu ya hao watoto, ndipo arobaini na wawili wa hao wakauawa na dubu, mnaona. Na huyo hakuwa ni Roho Mtakatifu, bali ilikuwa ni nabii huyo, aliyekasirika. Na mimi—mimi nimeyapitia mambo haya yote, kufikia hapo.

159 Basi huyo hapo alisimama, akisema nami. Ndipo akasema, “Lakini wewe unatembea na wengi kupita kiasi.” Akasema, “Kutembea pamoja Nami, utatembea peke yako.”

160 Nilikuwa nimeona basi, nilikuwa nikijishughulisha mno na madhehebu na kila kitu, mnaona, mtu fulani akijaribu kukwambia la kufanya na usilopaswa kufanya. Huna budi kumfuata Yeye. Sasa, kumbukeni lile ono alilonipa kuhusu wale samaki, mwajua, na jinsi ambavyo usingeweza kuwafundisha watoto wachanga wa Kipentekoste ishara za kimbinguni. Mnakumbuka. Basi hilo hapo. Nami niko tu kwenye kilele cha Ujumbe huu mpya.

161 Mara hilo ono liliponiacha, nikasema, “Amina, Bwana!” Naye mke wangu alikuwa amesimama pale, karibu azimie. Ndipo nikaruka kutoka kitandani, ningeweza kuzungumza vizuri kama nilivyowahi kufanya. Katika sekunde moja tu, kila chembe ya homa ikaniacha.

¹⁶² Nikampigia simu Doc Schoen, nikasema, “Ningetaka unichunguze.”

Akasema, “Ati nini?”

¹⁶³ Nami nikaja kule, naye akanichunguza, akaangalia kwenye huo uwazi wa pua, kasema, “Hebu niambie ni kitu gani kilichotukia, Ndugu Branham.”

Nami nikasema, “Ungeiamini hadithi yangu?”

Akasema, “Ningewezaje kuitilia shaka? Imetendeka.”

¹⁶⁴ Jambo ndilo hilo, mnaona. Jambo ndilo hilo, rafiki. Mungu anajua jinsi ya kukushikilia kwenye lundo la majivu. Yeye anajua jinsi ya kukufanya jambo fulani mpaka anapoweza kukuletea Ujumbe, unaona, kukufanya ufanye jambo fulani.

¹⁶⁵ Leo hii, sijui kushindwa kwingi. Niliingia sio muda mrefu uliopita, nilikuwa nikisikiliza tangazo la redio. Basi palikuwapo na mhudumu akihubiri juu ya ufufuo, kutoka kwenye Wakorintho wa Kwanza 15. Naye alikuwa akihubiri ufufuo. Ndipo akasimama moja kwa moja katikati ya mahubiri yake, na akasema, “Mnajua, watu wengi sana wanaogopa kushindwa.” Akasema, “Wakati Jemadari Patton alipopoteza kundi la askari,” kasema, “basi walimwambia... Aliagizia na alitaka wengine zaidi, nao wakamtumia wengine. Wakauawa, naye akaagizia wengine zaidi. Ndipo alipolipeleka hilo kundi la tatu kule juu,” kasema, “kila wakati risasi ingelia, wangekimbia chini ya bati, ama kukimbia chini ya kitu fulani, wameshikwa na woga.”

¹⁶⁶ Akasema, “Nitumieni wanaume, sio watoto.” Akasema, “Ninataka wanaume walio tayari kufa. Sitaki mtu anayeogopa kufa. Kama kanuni tunayopigania haistahili kufiwa, basi msiwalete kwangu. Ninataka wanaume.”

Wakasema, “Lakini umeshindwa mapigano mawili au matatu.”

¹⁶⁷ Akasema, “Sijapoteza vita. Nimepoteza tu mapigano.” Jambo fulani likanena moyoni mwangu.

¹⁶⁸ Ninakumbuka Eisenhower alisema, “Nilipopiga risasi, niliwaamuru nao wakaingiza risasi kwenye bunduki, waliivuta nayo ikafifia, haikufanya kazi,” kasema, “sikuondoka na kujisalimisha. Nilitupa hiyo risasi nje na kutia nyingine ndani, nikaijaribu. Kama haikufanya kazi, nilitia nyingine ndani, mpaka moja ikafanya kazi.”

¹⁶⁹ Hivyo ndivyo inavyopaswa kufanywa. Sijui itakavyokuwa. Lakini Mungu kama Hakimu wangu juu ya mimbara hii, sijui ni kushindwa mara ngapi na ni mapigano mangapi—mangapi nitakayopoteza, ila sitapoteza vita. Yeye aliniambia angekuwa pamoja nami. Nitasimama hata nitakapoiona huduma hiyo imethibitishwa na kuiona ikitenda kazi. Ninaanza asubuhi ya leo, kwa neema ya Mungu. Sijui kama itafanya kazi hapaa, kama

itafanya kazi mahali pengine, jinsi itakavyotenda kazi wala kile kitakachotukia. Bali nitashuka moja kwa moja kwenye mistari ya maombi, nikiwaombea wagonjwa, mpaka nitakapojua linalotukia. Nimeliona likitukia mara mbili ama tatu.

¹⁷⁰ Nimeliona likitukia katika nyumba ya Hattie. Ni wangapi waliopata kuisikia hadithi ya wale kuchakulo, na kuhusu yule msichana, mwanamke mdogo? Mtu wa kwanza katika wote tangu tumejua, tangu siku za wale wanafunzi, aliyepewa majaliwa ya kusema, “Omba utakalo,” wakati ukiwa pale. Mlipata kuisikia hiyo hadithi? Mlipata kumwona mwanamke huyo? Ni wangapi hawakumwona, na wanataka, wangetaka kumwona huyo mwanamke ambaye lilimfanyikia? Sisi . . .

Hattie, ungeweza kusimama? Huyo hapo yule mama.

¹⁷¹ Akisimama nyumbani mwake. Nikiisha kuwaona kuchakulo wanane, ambapo hapakuwapo na yeyote mahali popote, na, kusema tu neno, nao hao hapo wangekuwa wamesimama. Hiyo ni kweli. Hiyo ni, hao hapo. Nami nikasema, “Ni kitu gani kilichowafanya hao kuchakulo kuja pale?” akiketi mezani pake. Naye mama yake, Dada Wright, huyu hapa Ndugu Wright, alikuwa ameketi pale. Ni wangapi waliokuwa mezani, ni wangapi waliopo hapa asubuhi ya leo? Inueni mikono yenu. Vema, hao hapo, kote jengoni. Mnaona? Vema, walikuwa pale. Nami nikasema, “Siku moja . . .” Maskini dada yao kiwete ameketi pale.

¹⁷² Nikasema, “Halina budi kuja kwa ono, kadhalika, lakini siku moja litatokea tofauti.” Nilikuwa nikizungumza namna hiyo. Mara, kitu Fulani chenye upako (liachie watu hawa), kamwe sijawahi kuhisi upako kama huo. Mbona? Kwa sababu Hattie alisema jambo lifaalo.

¹⁷³ Nikasema, “Hao kuchakulo walitoka wapi? Hapakuwapo na yeyote pale, si hata mahali pao, kama tu juu ya nguzo ya simu papo hapo. Nami nililiona likitendeka mara nane moja kwa moja.” Ndipo nikasema, “Sijui walitoka wapi.” Nikasema, “Jambo pekee nijualo, ni kwamba Mungu alijaribu kuthibitisha Ujumbe kwa Ibrahimu wakati mmoja, Naye akanena kondoo dume akawa, kwa sababu Yeye alihitaji kondoo dume, kulithibitisha. Hapana shaka kwamba nilihitaji kuchakulo, kuwanena wangu. Naye akafanya hivyo mara nane moja kwa moja, ama mara saba moja kwa moja, hasa, mara saba moja kwa moja.” Kisha nikasema . . .

¹⁷⁴ Basi, Hattie, labda bila kujua yale huyo mwanamke aliyokuwa akisema. Angalieni jinsi lilivyowapita matajiri na wenye kiburi. Angalia jinsi lilivyopita kila kitu, na kumjia maskini mwanamke mdogo wa nchi ya kale pale.

¹⁷⁵ Nami nilikuwa na dola ishirini mfukoni mwangu, kumrudishia huyo mwanamke, ambapo, alikuwa ametoa nadhiri ya dola hamsini kwenye kanisa hili jipya lijalo. Wala sisemi hili

kumwaibisha; asingeweza kupata senti hamsini, kwa kweli, kutoa. Lakini, moyo wake ukiwa kwenye huu Ujumbe, yeye alitaka kufanya hivyo. Ndugu Neville, ninaamini, alikuwa amekubali, asingechukua hizo zingine, alimwacha tu atoe dola ishirini zake. Nami nilikuwa na noti mbili za dola kumi kila moja mfukoni mwangu, Meda alikuwa amenipa za kununulia vyakula, nami nikasema, “Nitamrudishia leo hii.”

¹⁷⁶ Ndipo nikawazia, kitu Fulani kikasema nami, kasema, “Yesu alimwona yule mjane akitia mapeni yake matatu, wala hakumrudishia.” Alimwacha aendelee kwa sababu alikuwa na kitu fulani kikuu zaidi chini safarini.

¹⁷⁷ Sikujua hata kidogo alikuwa akisema nami kwa njia iyo hiyo, ya mwanamke mjane, bila mume. Mumewe aliuawa. Wala mimi sikujua huyo alikuwa Ndiye yule yule, wakati niliposema, “Basi nitaweka tu hizo dola ishirini, Wewe una kitu kingine kwa ajili yake.”

¹⁷⁸ Nikasema, “Jambo pekee nijualo, ni kwamba Yehova angali ni Yehova-Yire. Yeye anaweza kutoa dhabihu.”

¹⁷⁹ Naye Hattie, pasipo kujua alilokuwa akisema, akasimama na kusema, “Hiyo ni kweli tupu, Ndugu Branham.” Loo, jamani! Hilo lilikuwa ndilo jambo linalofaa kusema. Hilo lilikuwa ndilo jambo linalofaa kusema.

¹⁸⁰ Yapata wakati huo, Nguvu za Mungu zilipagusa mahali pale; kamwe sijawahi kuhisi upako kama huo. Zilipofanya hivyo, nikasema, “Hattie, BWANA ASEMA HIVI, omba utakalo! Sijali ni nini, Mungu amenipa mamlaka ya kukupa shauku ya moyo wako sasa hivi. Ukiomba dola milioni moja, unaweza kuzipata. Omba maskini msichana huyo mdogo kiwete asimame na kutembea, ataupata. Omba lolote lile.”

Akasema, “Niombe nini, Ndugu Branham?”

¹⁸¹ Nikasema, “Lolote utakalo. BWANA ASEMA HIVI.” Loo, ni hisia ya jinsi gani!

¹⁸² Akaangalia pande zote. Huyu hapo baba yake mwenye umri mkubwa akiwa na mvi aliyekuwa amerudishwa kutoka kwa wafu, karibu hivyo. Huyu hapo ameketi mama yake mkongwe, mgonjwa. Huyu hapo ameketi dada yake mdogo, kiwete.

¹⁸³ Lakini alichagua kile kilichofaa tu. Alikuwa na wavulana wawili matineja kwenye umri huo tu wa kutokujali. Mumewe wa thamani ameenda Utukufuni; yeye alikuwa Mkristo, akingojea. Bali hao wavulana hawakuwa Wakristo. Akasema, “Nafsi za wavulana wangu wawili.” Mungu na aubariki moyo wake.

¹⁸⁴ Nikasema, “BWANA ASEMA HIVI, unao.”

¹⁸⁵ Nao hawa hapa, wamebatizwa katika hii Imani. Walikuwa wakiniambia hivi majuzi usiku, hata, yule mvulana mdogo sana akitawadha miguu mle ndani, akiweka mikono yake juu

ya kichwa cha Ndugu Neville, na kumwombea alipokuwa akitawadha miguu.

¹⁸⁶ Hao wavulana wawili wadogo huenda wameketi hapa mkutanoni mahali fulani asubuhi ya leo. Wako, Hattie, wako hapa pamoja nawe? [Dada Hattie anasema, “Wako huko nyuma.”—Mh.] Huko nyuma, nyuma. Mko wapi, enyi wavulana? Inueni mikono yenu. Wako wapi hao wavulana wawili? Hao hapo, wamesimama huko nyuma. Mungu awabariki. Vema. Haya basi.

¹⁸⁷ Sasa, ni jambo gani lililotukia? Jambo lile lile, haidhuru nini, ingekuwa kwamba yeye. . . kile angaliomba, angalikipata. Angalikipata.

¹⁸⁸ Sasa ninataka kuona hilo likitukia. Utakuwa ndio msimamo wa watu kwa Ujumbe. Mnaona vile alivyolisema? Alisema tu jambo lifaalo. Ni kile usemacho, ndicho kinacholitenda. Kile usemacho!

¹⁸⁹ Mwangalieni yule mwanamke Msirofoinike wakati alipomjia Yesu. Alisema, “Bwana, binti yangu amepagawa sana na pepo. Ewe Mwana wa Daudi, njoo ukamponye.”

¹⁹⁰ Akasema, “Si haki Kwangu kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia ninyi mbwa.”

¹⁹¹ Whiu! Vipi kama angalisema hilo kwa wengine wetu? Tunge sema, “Ati unaniita mimi mbwa? Huh, haikuwa kitu Kwake, kwa vyovyote vile! Kanisa hili kuu linasema kweli. Yeye si kitu ila mtakatifu anayejibingirisha. Yeye si kitu ila Beelizebuli.” Tungekuwa na msimamo huo. Bali si yeye.

¹⁹² Yeye alisema, “Ni kweli, Bwana. Umesema kweli kabisa. Ila mbwa wako tayari kula makombo chini ya meza ya watoto.”

¹⁹³ Hilo lilimpata. Akasema, “Kwa msemu huu, huyo ibilisi amemwacha binti yako. Kwa msemu huu!”

¹⁹⁴ Ni msimamo wako, enyi marafiki. Hivi Yeye hakusema hivyo? Hamna budi kuamini hilo, enyi marafiki. Ninyi, msiniamini, mimi ni mwanadamu; lakini aminini ninalowaambia, aminini Ujumbe. Usipomwamini mjumbe, uamini Ujumbe. Kama mtu aliingia mle chumbani, pamoja na barua ya simu, haidhuru ni nani, mtu huyo ana sura gani ama alikuwa ni nani, mkubwa ama mdogo, wewe amini kile kilicho kwenye hiyo barua ya simu, sio huyo mtu. Mungu alinituma kuwaambia. Ninao Ujumbe. Mungu alinituma kuwaambia ya kwamba Yeye amefufuka katika wafu, ya kwamba Yeye yuko hapa asubuhi ya leo. Amelithibitisha kwa ishara na maajabu, kwamba Yeye yuko hapa, na kila mmoja wenu anaweza kuponywa maradhi yako kama tu utachukua msimamo mzuri unapokuja. Utafanya hivyo, wakati tukiimba *Amini Tu*.

¹⁹⁵ Sasa hebu wale watakaombewa, waje moja kwa moja hapa juu na kufanya mstari papa hapa. Sasa, usije isipokuwa unaamini kwa moyo wako wote.

¹⁹⁶ Bwana wa thamani, saa ndiyo hii. Ninaomba ya kwamba utawaponya watu hawa, Bwana. Na kuyatakasaa mafuta haya. Jipatie utukufu Mwenyewe, Baba. Tunawatuma hawa katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹⁹⁷ Sijui kama tungeweza kuwaomba watu wale wanaosimama upande *huu* hapa, kama kunayo njia ambayo wangeweza kupata nafasi ndogo tu hapa, kusudi tuweze kuwapitisha watu huku, mkiweza. Moja kwa moja kupitia hapa, kutokea upande *ule*. Ndipo wote wanaweza kuja upande huu, kushuka moja kwa moja mstarini, kuufanya mstari unaotoka nje hivyo.

¹⁹⁸ Jambo fulani halina budi kutukia, Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasema, “Amina. Linatukia sasa hivi. Bwana asifiwe! Yesu yuko hapa. Naam. Kila mmoja wao ameponywa kwa Nguvu za Mungu.”—Mh.] Amina.

¹⁹⁹ (Wasemaje? Kweli. . . Vema, la, moja kwa moja upande ule. Mimi na Ndugu Neville, naam, tutawaombea moja kwa moja mwishoni. Kwa hiyo, hatuwezi kuwaleta huku hivi, maana ungeninii, ukifanya hivyo, utaninii. . . Hebu kidogo. . . ? . . .)

²⁰⁰ Sasa hebu niliambie kusanyiko linalongojewa: *Hili* ni Neno la Mungu, Yule ambaye mimi. . . Lile nimeliishia, na nitalifia, kwa neema na msaada wa Mungu. Mungu akiwa ndiye Hakimu wangu mwenye kicho, nimewaambia Kweli. Niliona, na mambo haya yote yakija kwake. Hata kuanzia maskini yule samaki mdogo aliyefufuliwa huko chini, mlipata kuisikia hadithi hiyo? Wale pale hao wanaume wameketi moja kwa moja huko nyuma, wote wawili, waliokuwa hapo wakati lilipotukia; lilisemwa siku moja kabla halijatukia. Sasa, ninawezaje kuwaambieni mambo haya ni nini? Mnaona, ninataka kuhubiri juu ya, moja ya siku hizi usiku, juu ya *Usawazisho*. Mwanadamu angeweza kukwambia jambo fulani, na aendeleo tu kujenga namna hiyo, bali ikiwa hakuna Maandiko ya kulisawazisha, hatimaye litaanguka chini. Kama vile upambanuzi huu, na maono haya na kadhalika ambayo nimewaambia habari zake, kama hiyo isingalikuwa ni Kweli; jambo la kwanza, kunayo Biblia ya kuliunga mkono, na kulikuwako na Roho Mtakatifu kuthibitisha kwamba nimewaambia Kweli.

²⁰¹ Sasa, nimekuwa na yapata miaka kumi na minne hudumani, kupitia kwa kila mkosoaji ambaye angeweza kupatikana mbele yangu. Wasomi, werevu, kila kitu kingine, hata wakati mmoja hawangeweza. . .

²⁰² Basi mnajua yale waliyosema? Mmeyesikia hapa. Wanasema, “Watu kusanyikoni watazunguka, waseme na watu.” Kwanza walisema ilikuwa ni watu kutoka kanisani mwangu,

wanaopanda kwenda kule kufanyiwa. Ndipo wasingewapata hao, kunao wengi wa hao kupita kiasi.

203 Jambo la pili walilosema, kwamba, “Ingekuwa kama ndugu” wanaoambatana nami, “wanasimama huko nyuma na kusema, ‘Mtu *huyu* anaweza kusikia, masikioni mwake.’”

204 Kisha wakasema ya kwamba, “Billy Paul, Billy Paul angekuja na—na kupanda kule juu na kusoma kwenye kadi, yale watu wanayosema. Kama kuna kasoro masikioni mwao, yeye angesema, ‘masikio yao’ ama ‘tumbo lao.’”

205 Ingewezekanaje kamwe kwa wale huko nje wasio na kadi za maombi? Kamwe ingewezekanaje kutabiri mambo yanayotukia kikamilifu? Ingewezaje kuwa hivyo? Isingewezekana. Mtu yeyote anajua, aliye na akili timamu.

206 Walisema jambo lile lile humhusu Yesu, hapo Filipo alipoenda akamleta Nathanaeli. “Yeye alikuwa ni rafiki wa Yesu.” Akasema, “Hakika, yeye alimwambia Yesu yote kuhusu hayo. Anaenda kumtafuta.”

207 Kisha hao wanafunzi wakasema, ama hao wanafunzi wa hilo kanisa kubwa walisema, “Mtu *huyu* ni Beelizebuli. Yeye ni Beelizebuli. Yeye ni mpiga ramli.”

208 Yesu alisema, “Nitawasamehe kwa ajili ya hilo. Lakini siku moja Roho Mtakatifu anakuja kufanya jambo lile lile, neno moja dhidi ya Huyu halitasamehewa kamwe.” Sasa kama . . .

209 Nimekuwa mwaminifu nanyi watu, mwaminifu nijuavyo mimi. Loo, huenda nilipinga baadhi ya imani mlizo nazo katika maskini thiolojia ndogo na kadhalika. Lakini, sababu ya mimi kufanya hivyo, Paulo alisema, “Kama malaika kutoka Mbinguni akija na kuhubiri jambo lingine ila lile Biblia ile isemalo,” na yale aliyofundisha, “na alaaniwe.”

210 Kwa hiyo, sina budi kufuata yale tu Biblia iliyosema. Kama Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana na milele,” ninaamini hilo. Yale tu Biblia iliyosema, hilo ndilo tu ninaloamini hasa. Ninalisema tu jinsi hiyo. Mimi sikuwa na elimu yoyote, sikuwa na mafunzo yoyote. Nilimsikiliza tu Roho Mtakatifu pamoja na Biblia. Na umbali huu, kufikia asubuhi hii ya Pasaka, kwa miaka thelathini na mmoja, kamwe hajaniaibisha.

211 Nami nawaambia ya kwamba Roho Mtakatifu aliniambia kuhusu huduma hiyo inayokuja, kwa miaka miwili ama mitatu iliyopita, nami nimekuwa nikiyaambia makanisa kila mahali. Naye Mungu Mwenyezi akiwa Hakim wangu, papa hapa juu upande huu wa Salem, hao kuchakulo wakawepo mahali ambapo hapana kuchakulo kabisa. Moja kwa moja kule chini tukiwa na Charlie, anayesimama huko nyuma, na wengi wao huku chini Kentucky; hao kuchakulo wakatokea moja kwa moja katika mahali ambapo hawakuwako, nikasema mahali wangekuwa. Ambapo Tony na hao wengine, Banks, wanaoketi

pale. Na hao hapo, kabisa. Nikarudi moja kwa moja, na mwanadamu wa kwanza liliyepata kunenwa juu yake, ilikuwa ni mwanamke yule anayeketi pale pale, na hilo hapo. Hivi majuzi asubuhi huko juu, nilipokuwa mgonjwa na huo ugonjwa wa koo, nilimwona Yesu amesimama mbele yangu, Naye akaniambia ya kwamba hii huduma tayari imethibitishwa kwangu.

²¹² Sasa yatakayotukia, sijui mimi. Lakini, jambo moja, sina budi kuweka kando hiyo nyingine, nipate kuingia kwenye hii. Jinsi tu nijuavyo kufanya. Na ijulikane sasa, hili na lichorwe, kama Ayubu alivyosema asubuhi ya leo, kwa kalamu ya chuma, mwambani. Sijui la kufanya. Jambo pekee nijualo, ni kupiga hatua mbele. Yeye aliniambia. Naye Mungu ndiye Hakimu wangu, aliniambia. Nimewaambia Kweli. Na iwapo Mungu amethibitisha na kuwaambia, wala hakuna wakati mmoja mtu yeyote hapa aliwahi kuweka mkono wao juu ya chochote kilichokuwa cha uwongo, basi hili ni kweli, pia. Ni kweli, pia.

²¹³ Sasa nikienda hapa na kusimama mwishoni mwa huu mstari, ninaye mzee, Ndugu Neville hapo, mtu mtauwa, mchungaji wetu hapa, kuwapaka watu mafuta, nitawawekea watu mikono, kwa sababu agizo la Yesu, baada ya Pasaka, lilikuwa, “Enendeni mkaweke mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.”

²¹⁴ Sijui atakachoniambia mstarini. Nitajaribu kuhisi upako ule mkuu. Sijui kitakachotukia. Sijui. Chochote kile, nitafanya jinsi tu Yeye anavyoniambia.

²¹⁵ Sasa njoni, njoni na moyo uliojaa. Haidhuru kama Yeye atakukemea, kama hakwambii lolote, haidhuru ni nini, wewe nenda ukimshukuru, unaona. Maana, kazi imefanywa, ni njia fulani ya kukupata.

²¹⁶ Sasa, ndugu, pamoja na huo mguu, ninakutaka uamini. Kama Yeye, kwa simu, angeweza kukuondolea ugonjwa huo wa tumbo, Hakika angeweza kukuondolea huo ugonjwa wa mguu asubuhi ya leo, unaona. Sasa amini kwa moyo wako wote.

²¹⁷ Naye yule mama aliyekuwa na mtoto huyo mchanga aliyekuwa na huo ugonjwa wa moyo, usitie shaka tena. Amini! Amini!

²¹⁸ Sasa nataka kila mtu kanisani awe katika maombi. Nami nitashuka niende kuomba. Nyinyi nyote iweni katika maombi sasa, wakati nikiupitisha mstari huu wa maombi, nikiomba, nikiweka tu mikono yangu juu pale na kutamka baraka.

²¹⁹ Na, kumbukeni, endapo mmoja wenu ana dhambi yoyote isiyoungamwa, na ijulikane kwenu ya kwamba Mungu kamwe hatawaponya mkiwa na dhambi hiyo isiyoungamwa. Isahihishe, kabla hujapitia hapa, maana huenda ikakufanya mbaya zaidi. Unaona?

220 Sasa si katika upambanuzi. Upambanuzi, ninayagundua mambo hayo. Lakini, na huu si upambanuzi, ninatafuta huduma mpya. Nyote mnaelewa vizuri? Vema. Sasa aminini.

Sasa na tuombe tunapoviinamisha vichwa vyetu.

221 Baba Mungu, alama za vidole vyangu zingali juu ya mimbara hii, tangu saa baada ya saa, kwa sasa karibu miaka thelathini ama zaidi, ambayo nimesimama hapa nikihubiri, na kote ulimwenguni. Nawe umeithibitisha Injili ambayo nimehubiri, kwa sababu huo Ujumbe ulitoka Kwako. Kamwe sikwenda kwenye shule zozote, kamwe sikumtaka ushauri mtu yeyote ila Wewe, nikilisoma Neno Lako na kungojea kuona yale Roho angesema lifanywe.

222 Na sasa, Bwana, Wewe unajua kuhusu huduma hii ya Marko 11:23, na nikijua ya kwamba saa imekaribia, nikijua ya kwamba nimesimulia kikweli juu ya hao kuchakulo, na kuhusu Dada Hattie na wavulana wake. Sasa, Baba, nikijua ya kwamba ono hilo lilinjia huko juu kitandani, hivi majuzi asubuhi. Niliiona Biblia hiyo, halafu ule msalaba, halafu Wewe. Nayo ilifunuliwa niani mwangu ya kwamba sina budi kuikubali, kwa kuwa imethibitishwa.

223 Sasa, Bwana, ninasonga mbele asubuhi ya leo kanisani mwangu, kusimama hapa asubuhi hii ya Pasaka, nikiomba ya kwamba utaniinua kwenye karama mpya, yenye nguvu zaidi, kwa ajili ya watu, yenye nguvu zaidi. Sio kwa sababu ya wokovu wangu; kwa sababu Wewe umeniokoa, bwana, tayari. Sio kwa ajili yangu binafsi; nimekataa mambo yote makuu, nipate kukujua Wewe. Kama ulivyoniambia mimi huko nje kwenye hekalu lile kuu, hivi majuzi, “Mimi ndiye fungu lako.” Sasa, Bwana, jalia niwe fungu Lako, kusudi nipate fadhili Kwako, Roho Wako apate kuingia ndani yangu. Ndipo ninapoweka mikono yangu juu ya watu hawa wa thamani wanaoteseka, jalia Roho Wako, Bwana, afanye kazi iliyosalia. Hivyo tu ndivyo ninavyojua kufanya, Bwana.

224 Ninakumbuka agizo langu, mimi “nilizaliwa kuwaombea wagonjwa, ukiwafanya watu wakuamini, na uwe mwaminifu unapoomba.” Bwana, mimi ninaninii tu... Sijui jinsi ya kuwa mwaminifu zaidi. Mimi—mimi... Wanateseka, Bwana. Nami ni—nimeteseka, mimi mwenyewe. Naomba, Mungu Mpendwa, jalia kwamba wataponywa, kila mmoja wao.

225 Ninaenda mbele sasa, Bwana, kwa imani, kama Musa alivyopiga hatua kuelekea kwenye Bahari ya Shamu. Ninatoka kwenye mimbara hii takatifu, nishuke kwenye mstari huu wa maombi, katika Jina la Yesu Kristo. Mungu aliyenipa kuchakulo hao, Mungu Yule aliyempa Dada Hattie maneno hayo, Mungu Yule aliyenifanya kuyanena, jalia aende pamoja nami. Ninaenda katika Jina la Yesu Kristo. [Ndugu Branham anaondoka kwenye

maikrofoni kuwaombea wagonjwa, mengi ya maneno yake hayasikiki vizuri—Mh.]

226 Shetani, ninahukumu ninii...wewe, katika Jina la Yesu Kristo, kumwacha mtoto huyu. Mwache, mtoke mtoto huyu; nenda zako, na mtoto apone.

227 Ninaweka mikono yangu juu ya ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo, na kuhukumu mateso ya mwili wake. Amina.

Katika Jina la Yesu Kristo, mpe haja yake.

228 Bwana, katika Jina la Yesu Kristo, mpe Dada Ruth uponyaji wake. Amina.

229 Nitamwombea huyu mtoto. Lakini na—nashuka kutoka kwenye mimbara ile...Unaishi wapi? [Dada huyo anasema, “Bloomington.”—Mh.] Bloomington, Indiana? Niandikie barua kuhusu mtoto huyu mchanga. Amevimba sana tumboni hapa sasa. Utaamini, mama, ya kwamba ni kweli? [“Ninaamini ni kweli.”]

230 Basi, Baba, ninaweka mikono yangu juu ya...mtoto huyu mchanga, na kumhukumu ibilisi huyu. Mwache huyu mtoto. Pia jalia...?...Jalia sasa awe mzima na mtoto aponywe.

Niandikie barua, katika siku chache.

231 Unamwona yule mtoto mchanga mwenye macho yenye makengeza aliye pale? Iwapo hutatilia shaka tena, utamrudisha mtoto *huyo* na kumwonyesha akiwa mzima na mwenye afya.

232 Ninaweka mikono juu ya dada huyu. Na awe na msimamo wa yule mwanamke Msirofoinike. Na jalia aponywe katika Jina la Yesu Kristo...?...

Jalia moyo uwe mzima, katika Jina la Yesu Kristo.

233 Ninasema maneno haya. Hana budi kuwa mzima. Haiwezi kuwa kitu kingine chochote. Yesu alisema, “Ninaweza, kama utaamini.” Sasa, kama Yeye anaweza kumfanya kuchakulo atokee moja kwa moja namna *hiyo*, kama alivyofanya kondoo dume wakati mmoja, Yeye anaweza kuufanya moyo huo uonekane wa kawaida na mzima. Hauna budi kuwa.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia moyo uwe mzima. Lijalie.

234 Sasa, hilo si ni rahisi? Ni rahisi. Mungu ni rahisi sana, tunapitia juu yake. Sasa wewe kuwa tu rahisi vya kutosha hata usiuwazie tena. Itakuwa sawa.

235 Bwana, jalia dada yetu aponywe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Dada...?...

236 Bwana, sasa nimeyasema maneno haya, kwa uaminifu kama ninavyoweza kuyakiri mbele za watu. Nimewaambia, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usitie shaka, waweza kupata uliyosema.” Katika Jina la Yesu Kristo, jalia mateso haya yaondolewe, na shida zote ulizo nazo. Usitie shaka sasa. Nenda papo hapo karibu Naye sasa.

237 Bwana, ninaweka mikono yangu juu ya mtoto huyu mdogo na maumivu haya makali ya kichwa. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

238 Bwana, katika Jina la Yesu Kristo, jalia mlima huo umwondokee, mjalie aponywe. Mjalie ndugu yetu sasa aponywe...?...Amina.

239 Kiziwi na bubu; bubukiziwi. Bwana, katika Jina la Yesu Kristo! Nimesimama na kuhubiri siku baada ya siku, na mwaka baada ya mwaka, Sijaona imani ikiwasiliana Nawe, maishani mwangu mwote, pasipo jambo fulani kutukia! Sasa, yeye ni kiziwi sikioni mwake, na henia tumboni mwake. Jalia aponywe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sasa, usitilie shaka.

240 Bwana, unayajua mateso ya mwili wake. Huku mikono ikiwa juu yake, kwa moyo mwaminifu, jalia aponywe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

241 Mauti yamekaa penye mlango mmoja, imani penye huo mwingine. Mungu, libingirishe hilo jiwe na ujalie imani itawale. Jalia kansa hiyo imwache, katika Jina la Yesu Kristo.

242 Bwana, jalia aponywe. Ninaweka mikono juu yake. Ule Ujumbe ungali unatangazwa kupitia kwenye kuta. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

243 Baba Mungu, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu. Na iwe, Bwana, Roho na nguvu Zako, kumjalia haja yake. Jalia iwe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Imekwisha. Usilitilie shaka sasa.

244 Bwana, shauku ya ndugu yetu ni kuja Mbele Zako, akiwa na ugonjwa huu juu yake. Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, jalia apate aombacho. Amina.

245 Ni jambo kuu jinsi gani! Jalia Roho Mtakatifu aje juu ya mtoto huyu, kwa utukufu wa Mungu wapate kumlea kwenye ninii yake...?...Kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, jalia aupokee. Amina.

246 Baba, katika Jina la Yesu Kristo, na iwe hivyo, ya kwamba dada yetu atapona, na ombi lake lijibiwe, katika Jina la Yesu. Amina.

247 Jalia litendeke. Utampokea Roho Mtakatifu. Hakuna njia ya kukuzuia...?...Huna budi! Huna budi kuupokea, maana Mungu alisema hivyo. Wewe simama Nalo.

Vunja utoke kwenye maskini ganda hilo hapo. Sema tu...?...

248 Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, ijalie haja ya dada yetu. Amina.

249 Baba, katika Jina la Yesu Kristo, ijalie haja ya dada yetu. Jalia aponywe. Amina.

250 Yeye anaweza kumfanya kuchakulo kuweko, mara saba mfululizo. Angempa mwanamke huyo chochote alichoomba; Yeye angekupa wewe...?...

251 Bwana, katika Jina la Yesu Kristo, ijalie haja ya dada yetu. Ni Neno Lako. Asante. Na ijaliwe kwake, Baba, kupitia Yesu Kristo. Amina.

252 Wapendwa wenu? Baba, katika Jina la Yesu Kristo, jalia hizi...?...

253 Bwana, maskini mwanamke huyu wa Kiyahudi... Wewe ni Mungu wa Ibrahimu. Ijalie, katika Jina la Yesu Kristo, haja yake. Na iwe hivyo!

254 Katika Jina la Yesu Kristo, Mungu wa Mbinguni, ijalie haja yake. Amina.

255 Msichana huyu mdogo. Ulipokuwa tu ukija jukwaani pale, Mungu alikuwa akiniambia yote kuhusu maisha yako. Atakuondolea huo wasiwasi.

256 Bwana, ninauhukumu wasiwasi katika msichana huyu. Jalia umwache saa hii na aondoke hapa mwenye furaha sana. Itakuwa, katika Jina la Yesu Kristo.

257 Mungu wa Mbinguni, uliyemfufua Mwanao, Yesu, katika huu ufufuo tunaosherehekea, naomba ausherehekee hata na zaidi leo...?... Katika Jina la Yesu. Amina.

258 Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninaweka mikono juu ya dada yangu, nikiomba ya kwamba aponywe sasa katika Jina la Yesu.

259 Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, jalia dada yetu aponywe. Amina. Hauwezi kumweka. Hauna budi kuondoka. Nenda, huu hauna budi kuondoka tu.

260 Bwana, katika Jina la Yesu Kristo, jalia dada yetu aponywe. Amina. Katika Jina la Yesu Kristo, ninamponya huyu, dada yangu. Amina.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamponya dada yangu. Amina.

katika Jina la Yesu Kristo, ninamponya dada yangu.

katika Jina la Yesu Kristo, ninamponya huyu, dada yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninampa haja yake. Amina.

261 Bwana, katika Jina la Yesu Kristo, ninampa maskini mama huyu haja yake.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninampa haja yake, Bwana.

Bwana, katika Jina la Yesu Kristo, ninampa haja yake.

262 Shetani, ninakutoa. Katika Jina la Yesu Kristo, mwache huyu mwanamke.

263 Alikufunga muda mrefu. Uko huru sasa. Utakuwa mzima. Itakuwa sawa sasa, basi. Liamini sasa.

264 Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ninampa dada huyu, ambaye ni kiwete, uponyaji wake. Amina.

265 Katika Jina la Yesu Kristo, ninampa dada huyu uponyaji wake. Amina.

266 Katika Jina la Yesu Kristo, dada, ninakupa uponyaji wako. Amina. Na iwe hivyo!

267 Ninatumaini kwa Mungu sifanyi kosa. Jalia hili, kwa imani. Na iwe hivyo!

268 Unaamini Mungu hukupa nguvu za kuponya ugonjwa wa moyo pia? Unaamini ile hadithi ambayo ndiyo kwanza nisimulie? Kwa moyo wako wote? Basi ninakupa uponyaji wako. Katika Jina la Yesu Kristo, ninakupa uponyaji wako.

269 Jina la mwanamke huyu ni nani ambaye ndio kwanza arudi hapa? Unaishi mahali fulani hapa? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Kumbuka ya kwamba umeponywa! Hiyo ni kweli tu kadiri ninavyosimama hapa.

270 Baba katika Jina la Yesu Kristo, ujalie huu, naomba, uponyaji wake. Amina.

271 Baba, katika Jina la Yesu Kristo, jalia apate uponyaji wake. Amina!

272 Na—na—nakutangaza... Ni—ni—ni... Kwa neema ya Mungu, kupitia kwa karama ya Kiungu, ninakupa uponyaji wako! Mwondolee mbali ibilisi huyo, pia.

273 Unaamini Dada Rose? Ee Bwana, Muumba wa mbingu na nchi, mpe huyu Dada Rose Austin uponyaji huu, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Haya basi, Dada Rose, enda ukiamini sasa.

274 Bwana, mpe dada yetu uponyaji wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina...?...

275 Unaamini hilo? Wewe amini kila chembe yake. Basi ninakupa, katika Jina la Yesu, haja yako. Mungu atamponya.

276 Na iwe hivyo, Bwana, kwamba ndugu yake ataponywa, kimwili na kiroho, katika Jina la Yesu Kristo. Amina!

Jalia hii iwe ndiyo ile saa ambapo...?...

277 Bwana, ninaweka mikono juu yake, wakati akiwa hana matumaini kabisa, kwa madaktari ama uponyaji wowote kutoka kwa sayansi ya tiba. Lakini sio kutokana na kukutana na Kristo aliyefufuka. Katika Jina la Yesu, jalia aponywe. Amina.

...?...

278 Bwana, mpe dada yetu, nikisikiliza kwa makini haja yake, nikiangalia kila neno alilosema. Ni kwa ajili ya Ufalme. Ninaomba kwamba Wewe utamjalia, katika Jina la Yesu. Amina.

[Dada mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]
...?...

279 Bwana, kama mtumishi Wako, nikimsikiliza mama huyo akimlilia mtoto wake mchanga, ninamhukumu ibilisi ambaye amefanya hili.

280 Na juu ya maungamo ya imani ya huyu mwanamke, ninamtoa pepo huyu. Hutaweza kumlemaza mtoto huyu. Ponywa katika Jina la Yesu. Amina.

Ndio kwanza anaponywa, dada. Usitilie shaka tu, hata kidogo. Mungu akubariki, ndugu. Huyu ni mtoto wako? Naomba ampokee Roho Mtakatifu!

281 Tafadhali mpeleke huyu mtoto mahali fulani na kumsikiliza kwa dakika chache tu. Ninaamini jambo fulani limetukia kwa huyu mtoto mchanga. Utaupokea. Unaamini hivyo?

282 Katika Jina la Yesu Kristo jalia ndugu yetu aupokee uponyaji wake.

283 Bwana, jalia Nguvu za Mwenyezi Mungu ziyahukumu mateso ya mwili wake, na kumjaza kwa Roho Mtakatifu. Hii ndiyo saa na wakati. Katika Jina la Yesu Kristo, ninampa yeye. Amina.

284 Sukari imekwisha. Ukampokea Roho Mtakatifu. Umeteseka muda gani...?...Maisha yako yote. Unaamini ya kwamba Kristo atakuponya na kukukomboza na mateso haya; akufanye mzima?

285 Mtoto wako? Mguu wa—wako. Umekuja tu peke yako? Kama ningalikuwa, kama—kama ningalikuwa na nguvu ndani yangu, unaona! Lakini ninaamini ya kwamba Mungu atanisaidia kuwa na imani kwa ajili yake. Nitafanya kila kitu kilicho katika nguvu zangu. Unaniamini? Unaiamini hadithi hiyo kuhusu wale kuchakulo? Unaamini? Unaamini kwamba inawezekana, kwamba asubuhi ya leo, ya kwamba Mungu angeweza kuuponya mwili wako, na utembeke tena, utembeke kama ulivyopaswa kufanya mara ya kwanza? Kuna jambo fulani lililotukia tu katika kuzaliwa kwako kule, kuna kitu ambacho kimekatiza kidogo kitu fulani nawe kamwe hukukua vizuri. Ni kama tu kiungo kikikua juu ya kiungo kingine, kinakishikilia chini. Vema, kama kiungo hicho kinaweza kutoka kwenye kiungo hicho, kitanyoka na kuwa sawa. Unaona? Hiyo ni kweli? Ni laana. Ni laana. Kama laana hiyo ingeweza kukuacha, basi utapona. Unaona?

286 Bwana, ninawazia, vipi kama huyu angalikuwa ni mtoto wangu, vipi kama huyu angalikuwa ni ndugu yangu? Kwa imani, ninaondoa hiyo laana, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

287 Bwana, ninaweka mikono yangu juu yake na kuuombea uponyaji wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

288 Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya mwanamke huyu anayeteseka, kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

Dada Nash, Mungu alikuokoa na kansa, miaka kadhaa iliyopita.

²⁸⁹ Bwana, mjalie Dada Nash haja yake. Kama mtumishi Wako, ninaomba hilo. Itatendeka. Hilo ndilo jibu, Dada Nash.

Katika Jina la Yesu Kristo, mpe dada yetu haja yake. Amina.

²⁹⁰ [Ndugu fulani na dada wanazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Asante, ndugu, basi rudi kwa watu wako waliokuwa pale. Mungu na alijalie. Wakati wa ajabu sana, watu wako walikusanyika wakati nilipokuwa kule. Ulikuwa huko Bombay tulipokuwa kule? Vema, basi unaamini mambo haya ambayo mimi . . . umeyasikia?

²⁹¹ Bwana, wakati akirudi kwa watu wake ng'ambo ya bahari, jalia aende amejazwa na Nguvu za Mungu, ameponywa kwa kila haja anayoomba. Jalia aende na kuipokea, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁹² Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, jalia dada yetu apokee haja yake.

²⁹³ Bwana, ijalie haja ya dada yetu. Jalia shida yake ikome sasa hivi, kwa ufufuo kupitia kwa Yesu Kristo. Amina. Dada, haina budi kutukia, haina budi kutukia tu!

²⁹⁴ [Dada mmoja anaongea na Ndugu Branham—Mh.] Unataka hili lirudiwe katika Injili? ["Naam."]

²⁹⁵ Bwana Mungu, wakati msichana huyu akisimama hapa, sio kwa malengo yoyote ya kichoyo. Anamwombea ndugu yake, ana uambukizi damuni mwake. Ninampa haja yake. Kwa agizo nililopewa na Malaika; na kwa ono la Yesu Kristo, majuma machache yaliyopita, chumbani mwangu; ninampa msichana huyu haja yake. Amina.

²⁹⁶ Haina budi kuwa. Unaishi karibu na hapa? [Dada huyo anasema, "Memphis, Tennessee."—Mh.] Memphis, Tennessee. Niandikie barua. Uta—uta—utapata haja yako.

²⁹⁷ Ndugu Grimsley. [Ndugu huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Mungu akubariki, Ndugu Grimsley.

²⁹⁸ Bwana, tunaweza kukumbuka ndugu huyu amekuja umbali gani, na shimo alimochongewa. Anataka Roho Wako zaidi, Bwana. Huyu nampa, katika Jina la Yesu Kristo. Tukiona kazi zake za nyuma, kwamba amejaribu kukufuata Wewe, basi, kwa Nguvu za a—agizo nililopewa na Yesu Kristo, likathibitishwa na Malaika pamoja na ono, ninampa Ndugu Grimsley shauku yake. Mjaze kabisa kwa imani, naye atakuwa na matembezi ya karibu.

²⁹⁹ Vipi kama nilikwambia, "Nenda zako ukaponywe, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu"? Unaamini yale niliyosema juu ya wale kuchakulo na mengineyo, na unaamini hayo kuwa ni kweli? Basi, Yeye, Yeye hunipa yale niuambiao "mlima"

huu...?...Hutakuwa na mwingine. Hutakuwa na mwingine. Hakutakuwako na ugonjwa tena, utakuwa yote mawili, mzima.

³⁰⁰ Ninampa, yeye, haja hii anayoomba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

³⁰¹ Baba Mungu, mjalie huyu, dada yetu, haja yake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sawa, dada, nenda, liamini.

³⁰² Baba, wakati mwanamke huyu akipitia hapa, ninaomba ya kwamba Wewe utampa haja yake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

³⁰³ Katika Jina la Yesu Kristo, ninampa mwanamke huyu haja yake. Amina. Usitie shaka.

³⁰⁴ [Dada mmoja anaongea na Ndugu Branham—Mh.] Unaamini utaipokea? [“Ndiyo.”] Basi ninakupa haja yako, kupitia kwa Nguvu nilizokabidhiwa kupitia kwa agizo la Yesu Kristo, na kushuhudiwa...?...Nenda, na—na Mungu atakuwa pamoja nawe.

³⁰⁵ Ndugu Fred, una nini moyoni mwako? [Ndugu Sothmann anaongea na Ndugu Branham—Mh.] Ndugu Freddie Sothmann, ninailaani hiyo sumu iliyoko mwilini mwako. Naomba iondoke, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

³⁰⁶ Ndugu Collins. [Ndugu Collins anaongea na Ndugu Branham—Mh.]

³⁰⁷ Bwana, ndugu huyu wa thamani anautafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Bwana, kwa yote yaliyo ndani yangu, ninatangaza Baraka hizi juu ya Ndugu Collins. Lijalie. Jalia Roho Mtakatifu aje juu yake, na jalia ajazwe na Roho Mtakatifu! Amina.

³⁰⁸ Ndugu Collins, huna budi kumpokea, hana budi kuja. Mungu hutujaribu tu.

³⁰⁹ Bwana, ijalie haja yake. Jalia akutumikie, na familia yake ikutumikie, kwa mioyo yao yote.

³¹⁰ Mungu, mjalie dada yetu haja yake. Kwa yote aliyoomba, jalia ayapokee, kupitia kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

³¹¹ Bwana, mpe ndugu huyu nguvu kulisaidia kanisa lake. Naomba hili lijaliwe. Ninampa nguvu hizi, kupitia kwa Yesu Kristo. Amina.

³¹² [Dada fulani anaongea na Ndugu Branham—Mh.] Dada, hicho ni kitu cha kuchukiza sana ulicho nacho, wasiwasi. Unaamini yale nitakayokwambia ni kweli? [“Ndiyo, ninaamini.”] Unaamini hilo sasa, ya kwamba ni—nilikwambia kweli? [“Ndiyo.”] Basi ninakupa uponyaji wako, kupitia Jina la Yesu Kristo. Kwa hakika tu kama ninavyosimama mimbarani, wasiwasi wako umekuacha.

³¹³ [Ndugu mmoja anaongea na Ndugu Branham—Mh.]...?... Inaonekana wazi, kote juu yako.

³¹⁴ Bwana Mungu, kwa maskini ndugu yangu wa thamani hapa, kilindi na vina vya roho yake vinaita kama kilindi kikiita Kilindi. Yeye anamtaka Roho Mtakatifu. Yeye ameiheshimu ibada Yako, Bwana, kwa kila njia aliyoweza. Kwa Nguvu za Roho Mtakatifu, jalia aje juu ya ndugu yangu, naye ajazwe na Nguvu na neema ya Mungu, Roho Mtakatifu. Mpokee, ninapomkabidhi katika . . .



ENENDENI, MKAWAAMBIE SWA60-0417M
(Go, Tell)

MFULULIZO WA UJUMBE WA PASAKA

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili ya Pasaka asubuhi, tarehe 17 Aprili, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org